*Watoto ni Muhimu - Shule ya Biblia*

Kitabu cha Mwalimu

UNIT 2



# MASHINE YA WAKATI

## Kitabu cha Mwalimu

*Kwa umri wote*

# Mashine ya Wakati




**Shule ya Likizo ya Kusoma Biblia kutoka kwa "Watoto ni Muhimu"**

**Kitabu cha Mwalimu**

**Kwa umri wote**

**Kitengo cha 2: Masomo 1-13**

**Wavuti:**

**www.ChildrenAreImportant.com/machine/**


## SHUKRANI KWA TIMU YOTE YA "WATOTO NI MUHIMU"

Mhariri na Kiongozi wa Timu ya Ubunifu: Flor Boldo

Waanzilishi: Dwight y Kristina Krauss

Mwandishi: Suzanna Kangas (Suki)

Timu ya Ubunifu: Jennifer Sánchez, Areli Salinas, Ramón Martínez, Marlon Hernández.

Msanifu: Julio Sánchez

Msimimamizi wa Usanifu: Suzanna Kangas (Suki)

Washauri: Mike y Vickie Kangas

Vielelezo: Lindy na Marafiki kwa ushirikiano na NosrettepArt

**www.lindyandfriends.com**

Linda P. Romero

Msimamizi wa Ukurasa wa Mashabiki: Verónica Toj

# Utangulizi

## KARIBU KATIKA SHULE YA BIBLIA, "MASHINE YA WAKATI" KITENGO CHA 2!

Timu ya Haki huwa inatumia Mashine hii ya wakati ili kusafiri hadi wakati uliopita katika maisha ya Yesu, huku ikishiriki wanayojifunza na jinsi matendo ya Yesu yanavyoathiri maisha ya timu hii na jamii ya kisasa. Katika mwongozo huu watoto wetu wataweza kujifunza na kutumia waliyojifunza katika sehemu ya "Haki", ambayo inatumika kisasa kulingana na somo kuu. Kwa mfano, kuwaona watu wote kama viumbe wa Mungu. Sehemu ya "Kazi ya ziada" inakubalisha watoto kufanya mazoezi kuhusu mambo wanayojifunza katika maisha yao ya kila siku. Kwa mfano: iwapo mtu atakukosea au kukudanganya, usipigane naye. Badala yake, kuwa mtulivu na kumwombea, huku ukimwomba Mungu kukupa amani. Zungumza na walimu wako wa Shule ya Jumapili ya watoto kuhusu jinsi ulivyohisi. Sehemu ya "wasifu" inawafunza watoto kuhusu ajira mbalimbali na jinsi zinavyoinufaisha jamii, kama vile jaji, umisionari, na mfanyabiashara, miongoni mwa nyinginezo. Baadhi ya ajira katika sehemu hii zinaangaziwa kwa namna isiyofaa katika mataifa tofauti kwa sababu ya jinsi watu wanavyotumia vyeo vya vya kazi kwa njia isiyofaa. Hii ni fursa yako ya kuwafunza watoto kuhusu namna inayofaa ya kutenda au ni nini ambacho Yesu angefanya katika hali kama hiyo. Nani anayejua? Labda mwanafunzi katika darasa lako atajiunga na ile ajira akiwa mtu mzima na aweze kufanya jambo linalofaa na kufanya kazi kwa ajili ya wema wa watu wengine badala ya kutumia mamlaka yake visivyofaa. Anaweza kuwa mwangaza wa Yesu katika jamii au nchi yake.

Pia, watoto wataburudishwa kwa sarakasi inayochekesha, mchezo, na kutatua mafumbo katika vitabu vya wanafunzi. Vijana wataweza kufikiria kuhusu sehemu ya maswali, ambapo azimio sio kupatiana jibu linalofaa, ila kuweza kwao kuishi maisha kama ya Kristo katika maisha yao. Uhudhiriaji unashinikizwa kwa kupata kadi mpya kila wiki.

Mwalimu, tuko na uhakika kuwa Mungu atazungumza katika maisha yako na yale ya wanafunzi wako katika kila somo, Anataka kuubadilisha ulimwengu, na hakuna njia nzuri zaidi ya kufunza kizazi kinachokuja! Fikiria ni nini kitakachofanyika katika jamii yako huku Mungu akifanya kazi katika mioyo ya watoto wenu na kuwasaidia kuwa karibu na wengine bila ubaguzi. Tunaomba kuwa Mungu atawabariki kwa kiwango kikubwa kwa kufanya kazi katika shughuli hii muhimu ya kuwafunza watoto.

Kwa upendo ndani ya Kristo. Timu bunifu ya Watoto ni Muhimu.



Dwight y Kristina Krauss — Flor Boldo — Suzanna Kangas (Suki) — Miguel y Vickie Kangas — Julio Sánchez — Verónica Toj

Areli Salinas — Ramón Martínez — Jennifer Sánchez — Marlon Hernández — Lindy & Friends — Los Niños Cuentan

# MUHTASARI

## 1 Jali kama Yesu

**Aliwalisha watu 4000: Mathayo 15:29-38**

Yakobo 2:15-16 "Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, 16na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?"

## 2 Bure kwa kila mtu

**Mwanamke katika kisima: Yohana 4:4-15**

Warumi 12:16 " Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi. Msinie yaliyo makuu, lakini mkubali kushughulishwa na mambo manyonge. Msiwe watu wa kujivunia akili.

## 3 Unafaa yote

**Kiongozi mchanga aliye tajiri: Marko 10:17-27**

Marko 8:35 " Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha."

## 4 Fuata maagizo ya Yesu

**Yesu aliwaponya watu 10 waliokuwa na ukoma: Luka 17:11-19**

Wafilipi 4:6 "Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu."

## 5 Kuwa mnyenyekevu kama Yesu

**Yesu aliwaosha mitume wake miguu: Yohana 13:3-17**

Wafilipi 2:3-4 "Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. 4Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine."

## 6 Enye upendo kama Yesu

**Yesu alipindua meza: Marko 11:15-17 (Yohana 2:13-17)**

Mathayo 23:13 "Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnawafungia watu ufalme wa mbinguni; ninyi wenyewe hamwingii, wala wanaoingia hamwaachi waingie."

## 7 Moyo wa Yesu kudhihirishwa

**Shamba la Gethsemane: Mathayo 26:36-39, 47-54**

Luka 6:27 " Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, Wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi"

## 8 Udhalimu!

**Yesu kuhukumiwa: Marko 14:57-65, 15:1-15**

Isaya 53:9 "Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake."

## 9 Uhai katika kifo

**Yesu Kusulubiwa: Mathayo 27:27-31, 45-54**

Isaya 53:5 "Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona."

## 10 Mtu asiyefaa kuokolewa

**Mwizi katika msalaba: Luka 23:32-33, 39-43**

Warumi 10:11 " Kwa maana andiko lanena, Kila amwaminiye hatatahayarika."

## 11 Siku mbaya zaidi kugeuka kuwa siku nzuri zaidi

**Ufufuo wa Yesu: Mathayo 27:57-61, 28:1-10, Luka 24:36-48**

Waebrania 11:1 " Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana."

## 12 Mtu asiyeweza kuamini

**Saulo aamini: Matendo ya Mitume 9:1-20**

Matendo ya Mitume 1:8 " Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."

## 13 Je, pia mimi naweza nikaja?

**Petero alihubiri kuokolewa: Matendo ya Mitume 2:14, 36-40**

Yohana 3:16 " Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."

# JINSI YA KUTUMIA NYENZO HII

## Sarakasi (Sehemu 1)




Katika kila sarakasi "timu ya haki" itarudi hadi wakati wa zamani ili katazama sehemu ya maisha ya Kristo, ambapo wanamemba wa timu wanasoma somo sambamba na kulitumia katika maisha yao ya kisasa. Sehemu ya kila sarakasi imeandikwa kabla ya somo kuu, ambapo wanarudi nyuma katika wakati, na sehemu ya pili ya kila sarakasi inakuja baada ya somo kuu, huku wanaoigiza wakirudi na kufanya walichosoma. Sarakasi hizi zimeundiwa waigizaji watatu: kiongozi, mchunguzi, na ajenti. Waagizaji wengine wawili, mekaniki na fundi, ni wa hiari iwapo uko na watu zaidi watakaojitolea.

## Somo kuu

Somo kuu linafuata sarakasi ya ufunguzi. Hadithi za Biblia hazijaandikwa kwa kamili katika somo hili, kwa hivyo tafadhali usisahau kusoma hadithi kutoka kwa Biblia.

## Sarakasi (Sehemu ya 2)

Baada ya somo kuu, kamilisha sehemu ya pili ya sarakasi, ambapo timu inasuluhisha tatizo kwa kutumia walichojifunza. (Tembelea kituo chetu cha YouTube ili kuona mfano)

Kiungo cha tovuti: https://www.youtube.com/watch?v=29oPA594_1s

## Haki

Fanya marudio ya sehemu hii fupi pamoja na somo kuu, huku ukitatua mafumbo katika vitabu vya wanafunzi, au huku ukikula vitafunio.

## Wasifu

Sehemu ya wasifu inawafunza watoto kuhusu ajira mbalimbali na jinsi ambavyo zinainufaisha jamii, kama vile kasisi, wakili, mwanasayansi, na polisi. Baadhi ya ajira katika sehemu hii zinatazamwa kwa namna isiyofaa katika mataifa tofauti kwa sababu ya watu kutotumia vinavyofaa vyeo vyao vya kikazi. Hii ni fursa yako ya kuwafunza watoto kuhusu namna inayofaa ya kutenda au ni nini ambacho Yesu angefanya katika hali kama hiyo. Nani anayejua? Labda mwanafunzi katika darasa lako atajiunga na ajira hii akiwa mtu mzima na aweze kufanya jambo linalofaa na kufanya kazi kwa ajili ya wema wa watu wengine badala ya kutumia mamlaka yake

visivyofaa. Anaweza kuwa mwangaza wa Yesu katika jamii au nchi yake. Ifanye kuwa inayoburudisha kwa kucheza mchezo mdogo inapoanza. Mwambie mtu kuiga ajira hii na uwaambie watoto kukisia ni ajira gani inayoigwa kabla ya kuwaambia.

## Aya ya kumbukumbu

Kila aya ya kumbukumbu inahusu somo lake. Zingatia kutafuta mchezo au shughuli ya kufanya ili ufanye ukariri kuwa jambo linalosisimua.

Tunapendekeza, "Michezo ya Aya za kumbukumbu" kama upakuaji wa bila malipo.

Kiungo cha Tovuti: http://www.childrenareimportant.com/myCMU/series/series-memory-verse-games.php

## Vitabu vya wanafunzi

Wanafunzi watafurahia kutatua mafumbo katika vitabu vya wanafunzi. Mafumbo ya kutafuta maneno na picha za kutia rangi zinaimarisha kila somo. Jadiliana maneno kutoka kwa mafumbo ya kutafuta maneno, kama vile thamani, unyenyekevu, na haki na uwaulize wanafunzi maneno haya yanamaanisha nini kwao.

## Maswali na majibu (wanafunzi wakubwa)

Maisha katika ulimwengu wa watu wazima ni mgumu. Je, si tungefurahia sana iwapo kungekuwa na mtu kila wakati wa kutupa majibu ya shida ngumu? Ila mara nyingi hayupo, na ni lazima tutafute majibu sisi wenyewe jinsi tuwezavyo. Wanafunzi wakubwa pia wanakaribia kuwa watu wazima. Iwapo kila wakati tunawaambia "majibu yanayofaa" kwa kila kitu na kukosa kuwauliza maswali magumu, watabaki kuwa wasio na mazoea na wasioweza kupata suluhu kulingana na Biblia kwa matatizo yao. Hili linawaacha wamechanganyikiwa na waliopotea wakati wanapopata maswali magumu na kupokea majibu ya kiulimwengu tu kutoka kwa wahadhiri wao au waliowaajiri. Badala yake, tumia sehemu hii ili kuwasaidia wanafunzi wakubwa kufanya mazoezi ya kufikirikia kwa kina. Anzisha majadiliano kati ya wanafunzi wakubwa. Usiwape "jibu linalofaa," ila waelekeze kwa upole ili waweze kupata suluhu nzuri kivyao. Tumewapa majibu kadhaa kwa maswali haya magumu kama mwongozo wa mwalimu.

## Mchezo

Cheza mchezo na wanafunzi! Michezo ni muhimu sana kwa wanafunzi, inawafanya waimarike katika ujuzi wa maisha ya kijamii. Vilevile, michezo inaburudisha! Hiki ni kifaa kizuri cha kuwahimiza watoto zaidi kuja na kusikia kuhusu Yesu, ambapo marafiki zao wote watakapowakaribisha katika darasa lako la kuburudika.

## Ratiba

**Fungua**

* Karib**Sarakasi na Somo**
* Sarakasi sehemu 1
*Somo
*Sarakasi sehemu 2

**Shughuli**

Do the biography and the justice section while doing other activities, such as the student's book or a snack. Fanya sehemu ya wasifu na haki huku ukifanya shughuli nyinginezo, kama vile kitabu cha wanafunzi
*Aya ya Kumbukumbu
*Vitabu vya wanafunzi
* Maswali na majibu (wanafunzi wakubwa)
*Mchezo (kwa hiari)

**Funga**

* Kazi ya ziada
* Kadi za usaidizi

## Kazi ya ziada ya kufanyia nyumbani

Maandiko yanasema kuwa basi muwe watendaji wa neno na wala msiwe wasikilazaji tu (Yakobo 1:22-25). Wafunze watoto kutumia neno la Mungu katika maisha yao ya kila siku kwa kutenda kulingana na jinsi walivyojifunza. Tumia dakika kadhaa kuwatuza kwa peremende au zawadi ndogo wanafunzi waliofanya kazi ya ziada ya wiki iliyopita.

## Kadi

Tumia kadi hizi kama tuzo ya uhudhuriaji. Kila kadi iko na umbo linalosisimua katika upande wa mbele na aya ya kumbukumbu katika upande wa nyuma.

# JALI KAMA YESU

01



### Kuwalisha Watu 4000: Mathayo 15:29-38

## SARAKASI (SEHEMU 1)

Mchunguzi alimwona mtu aliyekuwa akiomba katika barabarani kila siku ya wiki hii ambaye alikaa mdhaifu na mwenye njaa na mchafu. Anamwambia Kiongozi wa timu na Ajenti kuhusu mtu huyu na jinsi ambavyo amekuwa akimwombea kila wiki. Wanafikiria kuwa hili ni jambo nzuri. Wanapanda katika mashine ya wakati, na ikiwezekana, wanaitingisha mashine ya wakati na kufanya kelele za kiufundi huku mashine ikiwatuma nyuma katika wakati wa zamani kwa kipindi cha somo.

## SOMO

Umati mkubwa ulikuwa ukimfuata Yesu, huku ukimsikiza akifunza. Walitosheka sana kumsikiza Yesu na kumwona akitenda miujiza hadi walikosa kula na walihisi njaa. Yesu aliwahurumia.

Soma Mathayo 15:29-38

Kuhisi tu huruma ndani ya Moyo wake haikusaidia umati katika njaa yao. Yesu alibadilisha hisia zake kuwa tendo na akafanya muujiza ambao uliwalisha watu 4000 kwa vipande saba vya mkate na samaki wachache wadogo. Kila mtu alitosheka! Yesu aliwapa zaidi ya kidogo, alitengeneza zaidi ya kutosha.

Je, unawajua watu wanaofanya Moyo wako kuhisi huruma? Watu ambao wako na vichache kukuliko au wanaofinyiliwa kwa namna fulani? Kuwa na upendo kwa mtu mwingine kama Yesu huwa kila mara unakufanya kutenda. Nenda ufanye jambo kuhusu hili!

Shida nyingi za dunia ni kubwa na tunafikiria “siwezi kufanya jambo kuhusu shida hizi.” Ila tunaweza kupata angalau mtu mmoja ambaye tunaweza kumsaidia.

Na ni jambo linalotosheleza sana kuwapa baadhi ya upendo ambao Yesu anatupatia kwa kuwasaidia.

## AYA YA KUMBUKUMBU


*Yakobo 2:15-16 "Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki, 16na mtu wa kwenu akawaambia, Enendeni zenu kwa amani, mkaote moto na kushiba, lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini?"*

## SARAKASI (SEHEMU 2)

Baada ya somo kuu, timu inarudi katika wakati wa sasa na kutoka nje ya mashine ya wakati. Wote walishtuka kwa jambo walililoliona, jinsi ambavyo Yesu alizidisha mkate na samaki ili kuwalisha watu wengi sana. Hata wao walipata kukula baadhi ya vipande ambavyo vilianguka nyuma ya vichaka fulani (kwani wanajaribu kila wawezalo ili wasionekane ili wasivunje mwendelezo wa muda wa wakati). Mchunguzi anaiambia timu jinsi Yesu hakuwahurumia na kuwaombea tu watu waliokuwa na njaa, Aliwalisha. Anatambua kuwa anafaa kumsaidia mtu anayeomba anayemwona katika mtaa kila siku. Wanafikiria jinsi ya kusaidia, kama vile kumletea sandiwichi kutoka nyumbani au kutafuta kanisa karibu ambapo anaweza kumpeleka Yule mtu, na pia kuendelea kumwombea.

## HAKI

Yesu aliwapenda sana watu. Aliuhurumia umati uliokuwa na njaa na kuwalisha. Tunafaa kila wakati kujitolea kuwa wakarimu na kuwapa wengine.



## WASIFU (BOSI)

Bosi anafaa kusimamia shirika lote au sehemu ya shirika na kusimamia timu ambayo inafanya kazi pamoja ili kukamilisha majukumu, kuafikia malengo. Kuna mifano mingi ya mambo haya katika Biblia, kutoka kwa wafalme hadi kwa viongozi wa muziki, magavana, na mameneja wa miradi.
Majukumu: Bosi anafaa kuelewa malengo ya shirika na ni lazima aongoze timu yake ili kuafikia malengo haya. Kazi ya bosi ni kuhakikisha kuwa kila mtu anafanya kazi kwa umoja kupitia mifumo inayofaa na kwamba hakuna kitu kinachokuzuia kupata matokeo uliyoyapangia. Kazi ya bosi ni kulinda jina na sifa za kampuni, na pia kuzuia biashara kwenda katika mielekeo tofauti.
Fursa: Bosi anaweza kusoma kutoka kwa Mfalme wetu mkubwa jinsi ya kuwa kiongozi mtumishi.
Bosi mzuri huwa hatawali wafanyakazi ila atawahudumia. Bosi yuko na fursa kubwa ya kuwainua wafanyakazi kwa kuwatia moyo, kuwasifu mbele ya watu wengine, kutambua mchango wao na kazi yao nzuri ya kujikuza na kuimarisha ujuzi mpya, huku kila wakati akiangalia talanta asilia kutoka kwa wafanyakazi na kuwahimiza kuimarisha uwezo wao.
Msimamizi wa huduma atafanya kazi ili kulinda timu kutokana na mienendo ambayo itasababisha matokeo mabaya na kuwaongoza wafanyakazi wao changamoto binafsi, na wakati mwingine kufanya maamuzi magumu kwa nia njema. Bosi hufanya kazi ili kuwapa wafanyakazi wake zana, mafunzo na uhamasisho ili wafanye kazi yao vyema zaidi, na vile vile kuwapa fursa za kukuza na kuendeleza ujuzi moya, na kutafuta ujuzi asilia katika wafanyakazi na kuwahimiza waimarishe uwezo wao.

## MASWALI NA MAJIBU

1. Je, ni kwa nini mara nyingine siko mstarehevu na mambo ya Mungu?

Mara nyingi, tumezoea marafiki zetu kutufanya kuhisi vyema, bila usaidizi wao au kibali chao tutahisi hatuko wastarehevu mahali popote. Kumbuka ambacho maandiko yanatufunza katika 2 Timotheo 2:15 (soma kwa sauti kubwa) itakuwa vizuri zaidi iwapo utaanza kupokea kibali cha Mungu badala ya kutoka kwa marafiki zako, na unavyosoma neno zaidi na kufanya jinsi linavyosema, litakusaidia katika siku zijazo. Kuubadilisha hata mtazamo wako.

2. Je, unawezaje kuwaonyesha upendo wazazi wako na mamlaka?

Mungu anathamini sana kuwa tunafaa kufuata wanachotwambia wazazi wetu, ni amri ya kwanza iliyo na ahadi. Iwapo unataka sana kubadili mtazamo wako unaowaathiri visivyofaa wazazi wako, fikiria kwa muda ni kwa nini tumetenda hivyo, je, inakuaje naweza kuwaonyesha upendo watu wengine na sio wazazi wangu? Ni chaguo la kibinafsi kubadilika kwa mtazamo wa kibinadamu, iwapo tutakabidhi maeneo haya mikononi mwa Mungu, tutaweza kubadilika na kuweza kufarahia wakati tunaoutumia pamoja.

## MAJIBU YA MAFUMBO

### FUMBO LA KUTAFUTA MANENO

| | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | U | O | U | K | A | R | I | M | U | N | K | S | N | G | A | E |
| R | A | Z | I | J | U | U | M | L | I | A | E | J | L | Z | O | R |
| E | M | H | Y | P | R | F | G | E | I | U | A | T | I | S | E | T |
| M | N | U | E | E | A | L | I | S | H | A | N | J | N | H | M | U |
| A | U | N | S | K | Y | T | A | N | U | E | U | W | E | I | N | E |
| T | D | G | E | A | A | N | K | T | Y | I | S | M | P | D | T | O |
| O | Y | L | I | M | I | O | H | I | M | I | A | V | N | A | L | I |
| H | U | E | U | A | N | D | N | W | U | B | L | M | K | I | Y | Z |
| Y | B | S | A | M | A | K | I | E | A | K | U | I | N | T | N | K |
| I | A | A | E | U | T | N | K | Z | O | N | M | N | W | N | M | I |
| Z | K | T | H | Y | L | A | I | S | I | H | N | K | E | A | P | F |


**Tumia mojawapo ya maneno yaliyo katika orodha ili kukamilisha sentensi. Tia X katika maneno ambayo hayatatumika.**

*4000* *mkate* *mawe* *lisha* *huruma*

*hasira* *samaki* *wakati* *umati* *100*

Sikujua....


___*umati*___ mkubwa ulimfuata Yesu.
Yesu aliwalisha watu ___*4000*___,
Kwa vipande saba vya ___*mkate*___ na ___*samaki*___.
Yesu alikuwa na ___*huruma*___ kwa umati na aliwa ___*lisha*___.



## MCHEZO

***Salamu kwa kutumia mwili.***

Mwalimu anawaalika wanafunzi kuunda duara mbili, zikiwa na idadi sawa ya watu, moja ndani ya nyingine, na kuwaambia waangaliane. Waambie wapungiane mikono na kusema majina yao, vitu wanavyopenda na vitu ambavyo hawavipendi. Mwalimu anawapa ishara ya kuzungusha duara katika upande wa kinyume, kwa jinsi ambayo wakati inaposimama, kila mtoto yuko mbele ya mtoto mwingine. Mwalimu anawaagiza wasalimiane kwa kugongana viganja hewani, kujitambulisha kwa kusema jina lao na kuuliza maswali mengine. Kwa mfano, ulifanya nini wakati wa wikendi? Je, unapenda nini kuhusu mkutano? Halafu wanageuka tena na wakati huu wanapungiana kwa miguu, halafu viwiko vya mikono yao, mabega, n.k.






## KAZI YA ZIADA

Chagua mwenzako kutoka shuleni au eneo jirani ambaye ako na mahitaji.

Iwapo inafaa, waulize wazazi wako kukusaidia kuwaletea matunda, nafaka, au kitu cha kukula—ambacho kinamtosha yeye pamoja na familia yake. Beba vyakula zaidi katika mkoba wako ili kusambaza. Kumbuka kuwa unaweza kutenda jambo hili hata kwa mtu anayefanya usafi katika shule yako.

# BURE KWA KILA MTU 02



**Mwanamke katika kisima: Yohana 4:4-15**

## SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Mchunguzi alikutana na mtu hivi majuzi kutoka kwa upande mwingine wa mtaa. Anaiambia timu jinsi rafiki huyu mpya ako na dhana tofauti naye. Kitu ambacho alikijali kilionekana kutomwathiri rafiki yake, ila kitu ambacho hakikuwa muhimu kwake kilimkasirisha rafiki yake sana. Na rafiki yake mpya yuko na dhana tofauti kuhusu jinsi usafi wa kibinafsi unafaa kukuwa. Anataka kuzungumza kuhusu Yesu na rafiki yake, ila hajui jinsi ya kufanya hivyo. Wanarudi katika wakati wa zamani kuona miingiliano ya Yesu na mtu aliye tofauti sana Naye.

## SOMO

Wayahudi na Wasamaria walikuwa maadui waliokuwa na mambo yaliyofanana ila hawakutaka sana kukubali jambo hili. Walikuwa jamaa kutoka kwa mababu wamoja, na waliamini angalau vitabu 5 vya kwanza vya Biblia! Na vilevile, wote walikuwa watu walioumbwa na Mungu! Ila hawakusikizana, sanasana kwa sababu watu waliawaambia kutofanya hivyo. Hatujui ni kwa nini. Hivi ndivyo ubaguzi huwa unafanya kazi.
Yesu anampenda kila mtu na hakuogopa kuzungumza na mwanamke Msamaria. Pia hakuogopa watakachodhani watu wengine kuhusu jambo hili.
Soma Yohana 4:4-15
Hadithi hii sio kuhusu maji yanayoweza halisi. Katika hadithi, Yesu hakupokea maji aliyoyaomba. Anaweza kuwa alipokea, ila sio muhimu katika hadithi hii. Kilichokuwa cha muhimu ilikuwa ni Yesu kumpa "maji ya uzima" mwanamke huyu. Yesu alikuwa akizungumzia wokovu na maisha ya kuridhisha ambayo tuko nayo ndani ya Yesu, na Anampatia kila mtu. Je, unataka aina kama hii ya maisha? Usiwahi kuwa na kiu na kuwa huru kutokana na kiu cha mengine? Haijalishi wewe ni nani, Yesu anakupa maji haya!!!

## AYA YA KUMBUKUMBU

*Warumi 12:16 " Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi. Msinie yaliyo makuu, lakini mkubali kushughulishwa na mambo manyonge. Msiwe watu wa kujivunia akili.*

## SARAKASI (SEHEMU 2)

Watakaporudi, wanazungumza kwa furaha kuhusu jambo waliloliona, jinsi ambavyo Yesu alizungumza na mwanamke huyu ambaye baadaye aliongoza jiji lote kuja kumwona Yesu. Halafu wanatambua kuwa zawadi ya Yesu ya maji ni maisha kwa kila mtu, na haijalishi ni akina nani au wanakotoka. Mchunguzi anahimizwa kuwa anaweza kushiriki upendo wa Yesu na rafiki yake mpya na anapanga kufanya hivyo wakati ujao.


## HAKI

Yesu hakuogopa kuingiliana na watu ambao ulimwengu ulikuwa umewakataa. Basi kuwa kama Yesu na uzungumze na mtu ambaye mara nyingi hutaki kuongea naye kwa sababu ya hadhi yao katika jamii.

## WASIFU (BIBI WA NYUMBANI)

Mwanamke anayefanya kazi za nyumbani anaitwa bibi wa nyumbani. Ni kuhusu mtu ambaye anafanya kazi ambazo zinafaa kukamilishwa katika shughuli za kila siku za nyumbani.

Majukumu: Bibi wa nyumbani anasimamia usafi wa nyumba, kufua mavazi, mapishi, kununua bidhaa zinazohitajika na, iwapo yuko na watoto, anawatunza na kuwasaidia kusoma, na majukumu mengineyo zaidi. Licha ya kuwa na mujukumu haya yote, kazi yake haipokei malipo, kama mtu mwingine aliye na majukumu ya kikazi nje ya nyumbani.



Fursa: Mwanamke anayekaa nyumbani na watoto anaweza kutumia uwezo na uhodari wa watoto wake, na kuwafanya kuelewa na kuwafunza maadili, kanuni, na neno la Mungu. Ni fursa kubwa ya kusaidia katika maisha watu wanayoyaishi sasa.

Kwa wakati huu, tunafaa kuelewa kuwa kwanza sisi ni watu, mbele ya wanaume na wanawake, na kuwa sisi wote tunafanya mambo nyumbani kwa majukumu kulingana na uwezo ambao Mungu ametupatia. Tunafaa kujiamini sisi wenyewe na kupokea kusudi la Mungu katika maisha yetu.

## MASWALI NA MAJIBU

1. Je, naweza aje kuwa na uhusiano mkubwa na watu ambao siwapendi?

Hata kama tunafikiria ni ngumu, sio ngumu kama jinsi inavyokaa kusikizana na watu ambao hatuwapendi. Wakati mwingi, hatumpendi mtu kwa sababu tu marafiki zetu hawampendi pia, ila hatujafanya jaribio la kujua huyu mtu. Ni fursa kwako kufanya mambo kwa namna tofauti.

2. Je, na iwapo nitajihusisha na mtu ambaye hayuko na sifa nzuri vile?

Katika historia wanatwambia kweli kuhusu mwanamke Msamaria, mwanamke ambaye jina lake halijulikani, ila sifa zake zinajulikana. Hata hivyo, hili halikuwa kisingizio kwa Yesu kukosa kumpatia mpango wa wokovu. Jinsi tu ambavyo tunaweza kukataa kuzungumza na mtu kwa sababu ya kile watu wengine watakachosema, tnaweza kuamua kuzungumza na watu ambao watu wengine hawataki kuzungumza naye; tunaweza kupata mshtuko mkubwa.


3. Je, nafaa kuiga kila kitu alichokifanya Yesu?

Kwa ujumla, matendo ambayo aliyafanya ni ambayo yanafaa kutuongoza, haimanishi kuwa tunafaa kufanya mambo jinsi alivyoyafanya, ila yanafaa kuwa rejeleo la kutuwezesha kufanya maamuzi katika tabia yetu. Paulo anatuhimiza kumwiga, kama jinsi anavyomwiga Yesu (1 Wakorintho 11:1), mojawapo ya nukuu ambayo tunaweza kuitaja kuhusu jambo hili, Wafilipi 2:3-8, tunafaa kuwa na mtazamo wa kuwafanyia watu wengine mazuri bila kunufaika kwa namna yoyote.

## MAJIBU YA MAFUMBO







## MCHEZO

***Ishara na salamu***

Kiambie kikundi chote kuunda mduara. Mtu anaanza kwa kusema jina lake na baadaye ishara, kuruka, salamu, kudensi, n.k. na kila mtu anarudia. Endelea hadi kila mtu aseme jina lake kwa ishara yao na kikundi chote kimerudia.






## KAZI YA ZIADA

Ingiliana na mvulana au msichana aliye na shida katika chumba cha shule yako, au na mvulana mhamiaji au anayetoka kwa dini nyingine. Usikubali ubaguzi kukuzuia. Msalimie asubuhi na umuulize jinsi siku yake ilivyokuwa. Iwapo utaweza, mgawie chakula chako na usisashangae akikataa. Jaribu jambo hili katika wiki halafu uzungumze na mwalimu wako wa Shule ya Jumapili kuhusu jambo lililofanyika.

# UNAFAA YOTE

03



## Kiongozi Mchanga Tajiri: Marko 10:17-27

### SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Ajenti anasema kitu ambacho kimekuwa kikimsumbua kwa muda. Amekuwa na mchezo anaoupenda wa video ambao anaucheza kila anapopata wakati. Una mburudisha sana anaweza akaucheza kwa masaa mengi, na anaimarika sana katika mchezo huu na anaweza akashinda vita vikubwa na vikubwa zaidi na ameweza kushinda vikombe vingi na vifaa maalum, vingine ambavyo ni adimu sana. Hata hivyo, mchezo huu umekuwa ukimsumbua kwa sababu kuna mitazamo fulani katika mchezo na hata maovu yaliyomo katika mchezo huu ambayo anajua rohoni mwake kwamba ni mabaya. Ila inakaa kama burudani isiyo na madhara. Bado anaweza kukamilisha kazi yake yote ya ziada ya shuleni akiwa nyumbani na pia kazi za nyumbani. Anacheza tu wakati ambapo yupo na wakati wa kupumzika. Timu inashangaa kiasi kuhusu analofaa kufanya. Wanaamua iwapo wanaweza kujifunza kitu kwa kurudi katika wakati wa zamani.

### SOMO

Mungu hataki kitu chochote kuingilia kati Yake nasi. Anatupenda sana hata anaweza kuja kwetu kama mtoto ili Aweze kuhisi tunayoyapitia katika ulimwengu wetu na kupatana nasi tunakoishi! Wacha tuangazie hadithi hii.

Soma Marko 10:17-27

Mtu Yule tajiri alipomwuliza Yesu alichokihitaji ili kuokolewa, Yesu aliona kuwa Yule mwanamume alipenda sana utajiri zaidi ya uhusiano wake na Mungu na Yesu aliaangazia kitu hichi kimoja. Yesu alimwambia akauze mali aliyomiliki na kuwapa pesa masikini pesa hizi baada ya kuuza mali. Ila Yesu alisema kweli, huyu mwanamume hangeuza mali yake. Utajiri wake ulikuwa muhimu sana kuliko uhusiano wake na Mungu.

Je, ni nini cha muhimu sana kwako? Fikiria kuhusu kitu cha muhimu sana kwako zaidi ya Mungu. Je, anaweza kupatia kifaa chako cha kuchezea? Au uko tayari kuiacha familia yako siku fulani na kufanya anayotaka Mungu?

Mungu anataka uhusiano wa kibinafsi na kila mmoja wetu sana hivi anahisi wivu iwapo kitu chochote kitakuja kati yetu na Mungu. Pesa, sifa za umaarufu, marafiki, na hadhi za kijamii ni mambo ambayo yanaweza kuwa vizingiti kati yetu na Mungu.

Lengo la Mungu sio kutunyima vitu vizuri, ila kutupa maisha yaliyojaa neema tele pamoja Naye. Na vitu hivi vinaweza kuingia kati yetu Naye.

### AYA YA KUMBUKUMBU

*Marko 8:35 " Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha."*

## SARAKASI (SEHEMU YA 2)

Wanaporudi, ajenti anaiambia timu kuwa sasa ni wazi mambo tunayofaa kufanya. Hata ingawa anahisi kuwa mchezo huu unamburudisha na unatuza na yuko na ameweza kupata hazina nyingi, hakuna kitu ambacho ni muhimu kuliko kumfuata Yesu. Labda anaweza kucheza mchezo tofauti wa video ambao unamtukuza Mungu zaidi, ila anajua ni lazima awache kucheza mchezo anaouenzi sana. Kiongozi anapendekeza kuwa iwapo anataka kuacha kucheza mchezo ulio na uraibu, anafaa kuutoa kabisa kutoka kwa kifaa chake ili kuzuia ushawishi. Ajenti anakubali na anaamua kufanya hivyo pindi tu anapofika nyumbani.

## HAKI


Ukimwona mtu yuko na vitu vichache na pesa chache kukuliko, kumbuka kuwa kuna vitu vichache kati ya huyu mtu na Mungu.

## WASIFU (MFANYABIASHARA)

Mfanyabiashara ni mtu ambaye anajihusisha na mashauriano ya kibiashara, ununuzi, uuzaji wa bidhaa. Jina hili linatumika kwa mtu ambaye yuko na biashara au anayefanya kazi katika biashara.

Majukumu: Wanahakakisha jamii zinapata bidhaa za kimsingi na hata dawa zinazohitajika, pamoja na vitu vinginevyo. Ni jambo la kusisimua kujua kuwa wafanyabiashara wanafanya moja kati ya shughuli za zamani sana hapa duniani.

Fursa: Wafanyabiashara ni watu ambao wananunua au kuuza bidhaa. Hivi wanaingiliana na watu wengi wa jiji au mji. Ni muhimu kuwa mtu mwaminifu na kumfunza kila mteja jambo mnapojadiliana naye. Hii ni njia nzuri sana ya kusambaza neema ya Mungu katika maisha yako, ili imani ya watu wengine iweze kukua unapopatana na mtu ambaye ni shahidi wa uaminifu wa Mungu.



## MASWALI NA MAJIBU

1. Je, ni lini mwisho ulifikiria kuwa mipango yako ilikuwa muhimu zaidi kuliko kumtukuza Mungu?

Ni ngumu kuelewa aliyotupangia Mungu katika maisha yetu. Tunaweza kusema kuwa ni ngumu kuamua kumtumikia Mungu au kufuata ndoto zetu. Tunapojaribu kutizama mambo jinsi ambavyo Mungu anavyoyatizama, mtazamo wetu unabadilika. Kufanya hivyo sio kutupilia mbali ndoto zetu; ni kukubali mpango wa Mungu katika maisha yetu. Abrahamu alifanya maamuzi ambayo yalikuwa muhimu, kuacha kila kitu na kwenda mahali ambapo hupajui. Ila alikuwa na imani ya kutumaini kuwa mpango wa Mungu ulikuwa mzuri zaidi na kwamba ndoto zake zingeweza kutimia kwa kufanya alichoamuru Mungu baba.


2. Je, ushawahi kujishurutisha kuonyesha upendo wa Mungu kwa namna yoyote?

Tunapothamini mambo ya Mungu na kuyafanya kutoka ndani ya roho, ni kitu ambacho kinaonyesha shukrani zako na upendo kwake. Tunasema kwa matendo yetu kuwa tuko tayari kumtumikia Mungu. Kwa mfano, Yule mwanamume tajiri hangetengana na utajiri wake kwa sababu utajiri huu ulikuwa ndio kitu cha muhimu sana kwake.


3. Je, naweza kujua aje anachotaka Mungu katika maisha yangu?

Kumwomba Mungu kila siku tunaweza kuelewa anachotutaka kufanya au jinsi ya kutenda. Kumbuka kuwa, anataka kuwa na uhusiano wa kibinafsi nawe na kuondoa katika maisha yako kitu chochote ambacho kinaweza kuwa kizuizi kati yako naye. Usijilinganishe na watu wengine; Mungu anatenda kibinfasi. Kila mara kusudi lake katika maisha yetu ni zuri kila siku katika vipengele vyote vya maisha yetu.

## MAJIBU YA MAFUMBO










## MCHEZO

### *Mchezo wa Ndimu*

Wagawanye watoto katika vikundi viwili. Weka ubao au karatasi kubwa umbali mdogo kutoka kwa mstari wa kuanza. Mpatie mtoto wa kwanza katika kila timu penseli na kijiko. Anafaa kushika kijiko na mdomo wake tu, huku akibeba ndimu. Kiongozi atakaposema "nenda" anafaa kwenda kwa ubao bila kuangusha ndimu na kuandika neno la kwanza katika aya ya kumbukumbu. Halafu anafaa kurudi katika timu yake na kumpatilishia mchezaji anayefuata penseli na ndimu. Timu ya kwanza itakayomaliza kuandika aya yote ya kumbukumbu, ikiwa ni pamoja na rejeleo, itashinda.






## KAZI YA ZIADA

Chagua moja ya vifaa vya kuchezea au kifaa ambacho unafikiria unakithamini sana (iwapo unataka sana kufanya jambo hili) na kukipa mtu ambaye hana vifaa vingi vya kuchezea. Iwapo ilikuwa ngumu kwako kufanya hivyo wiki hii, jaribu tena wiki inayofuata. Baada ya kufanya hivyo, waambie wanafunzi kati ya wenzako katika masomo ya Jumapili ya watoto. Je, ulikuaje?



**Yesu aliwaponya watu kumi waliokuwa na ukoma: Luka 17:11-19**

## SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Ajenti anakuja na kuomba timu usaidizi. Anasema kuwa wazazi wake wametambua mabadiliko makubwa katika tabia yake baada ya kukubali Yesu, jambo ambalo ni nzuri. Ila hawezi kuacha kusema maneno mabaya; yanamtoka tu. Je, kuna kitu ambacho anaweza kufanya ili kuacha jambo hili? Mchunguzi anawaambia jinsi anavyong'ang'ana kufanya kazi za kinyumbani na mara nyingi hazifanyi, jambo ambalo sio sahihi kwa mama yake, na mchunguzi anataka kuimarika. Wakati mfupi uliopita, aliweka Biblia kando yake katika kitanda na kuisoma Biblia kila asubuhi na kuomba na kumwimbia Mungu wimbo hata kabla ya kutoka kwenye kitanda. Ni rahisi, ila anaendelea kuimarika katika kufanya kazi za kinyumbani kwa sababu wakati na Mungu umemsaidia kuanza asubuhi kwa mtazamo mzuri. Ajenti anaamua kuwa pia atajaribu jambo hili. Mchunguzi anamhimiza kuendelea kufanya hivyo kwa wakati mrefu, kwa sababu mabadiliko yanaweza kuwa taratibu. Wanarudi kwa wakati unaofaa kwa utume wao.

## SOMO

Sasa, Yesu yuko na upendo kwa "wageni." Watu walihisi kuwa Yesu hafai kuwa na uhusiano na watu hawa, ila Yeye, hata hivyo, aliwapenda na kuwaponya.
Soma Luka 17:11-19
Hakukuwa na sherehe au ibada au maombi maalum. Yesu aliwapa maelekezo kuwa wanafaa kwenda kwa makasisi ili kufuata amri katika agano Kuu la Biblia. Huku watu hawa kumi wakienda kufanya jinsi walivyoagizwa na Yesu, walipona ugonjwa huu. Kufuata maagizo rahisi ya Yesu kulisababisha baraka kubwa katika maisha yao.
Mmoja wa wanaume hawa alirudi kwa Yesu na Kumwabudu, huku akimshukuru Yesu kwa baraka hii. Ni rahisi kukubali tu baraka ya Mungu katika maisha yetu na kukosa kumshukuru Mungu! Hivyo, tunaweza kusoma angalau mambo matatu kutoka kwa hadithi hii. Kwanza, ni SAWA, kumwomba Mungu vitu tunavyovihitaji, hata ingawa tunahisi kuwa hatufai kupokea baraka yake.
Pili, Mungu anapotupatia maagizo, tunafaa kuyafuata maagizo haya.
Tatu, tunafaa kumshukuru Mungu kila wakati na kuwaambia wengine jinsi ambavyo alivyotutendea Mungu!

## AYA YA KUMBUKUMBU

*Wafilipi 4:6 "Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu."*

## SARAKASI(SEHEMU YA 2)

Kurudi kutoka kwa misheni, wanashtushwa sana na jinsi Yesu alivyowaponya watu waliokuwa na ukoma kwa namna isiyo ya kawaida. Ajenti anataja kuwa kufuata maagizo rahisi kunaweza kuleta mabadiliko makubwa.

Mchunguzi anatambua kuwa anafaa kumwabudu na kumshukuru Mungu huku Mungu Akiendelea kubadilisha maisha yake na kumtia nguvu ya kufanya kazi za nyumbani ili kumsaidia mamake. Kiongozi anataja jinsi ambavyo ameona mabadiliko yanayofaa katika maisha yao wote wawili na anamwabudu Mungu kwa mambo haya.

## HAKI

Angalia mambo anayoyafanya Mungu katika maisha ya watu wengine na usherehekee pamoja nao!


## WASIFU (MWUGUZI)

Mwuguzi ni mtu ambaye anawashughulikia au kuwasaidia wagonjwa, waliojeruhiwa, walioumia au wanaofariki. Mwuguzi anafaa kufuata maagizo ya daktari. Mwuguzi anawatunza watu wa umri wote anapoambiwa kufanya hivyo, peke yake au kwa kushirikiana na timu ya matibabu.

Majukumu: Kazi yake inahusu utunzaji wa moja kwa moja na wa kina wa wagonjwa popote ambapo wapo. Kazi yao ni muhimu sana ili kuendeleza afya na ustawi, na kuimarisha ubora wa maisha ya wagonjwa. Mwuguzi ni lazima asimamie kwa utiifu kwa maagizo ya kimatibabu na lishe bora inayofaa katika kila hali.

Fursa: Kwa kupata imani ya watu ambao wanawatumikia wanayagusa maisha yao kwa kiwango kikubwa. Zaidi ya ujuzi wa kiufundi na kinadharia, ni lazima wawe na mtazamo wa kuwatumikia wengine katika kazi hii ya wito. Inahitajika kuwa na ustahimilivu mkubwa na huruma nyingi kwa wagonjwa, kwa kuwezesha wengine kupata ujuzi wao, kujitolea kwao na umoja wao.

## MASWALI NA MAJIBU



1. Je, ni lazima nifuate maelekezo?

Nafaa kukumbuka kuwa kila wakati ambapo niko na kifaa au mchezo mpya, nafaa kusoma maagizo jinsi ya kupata mambo mengi kutoka kwa jambo hili. Hivyo naelewa kuwa maagizo ni muhimu, Yesu alimwambia Batimayo aende katika kisima na kuosha matope aliyokuwa ameyaweka juu ya macho yake, Batimayo aliyafuata maagizo yake na kupokea tena uwezo wake wa kuona. Tafakari ni nini ambacho kingefanyika iwapo hakufuata maagizo haya. Ni vizuri kujua kuwa aliyafuata na kuwa mwenye afya tena.

2. Je, ni kwa nini wazazi wangu wanasema ni lazima niwe mtu wa shukrani?

Ni mtazamo ambao tunafaa kuwa nao kila siku, labda kwako ni jambo ambalo linakukasirisha unapowasikiza wazazi wako au mamlaka inayokushauri kuwa mtu wa shukrani. Fikiria wakati katika somo hili ambapo tulisikia kuwa Yesu aliwaponya watu 10 waliokuwa na ukoma na ni mmoja tu, alipogundua kuwa amepona, alirudi kumshukuru kwa muujiza huu. Yesu anamwuliza: wako wapi hao wengine, je, si ni watu kumi ambao niliwaponya? Hili linatuonyesha kuwa, lilikuwa ni jambo nzuri kwake kurudi kutoa shukrani, ni muhimu pia sisi tuwe watu walio na shukrani.


3. Je, iwapo maagizo ya wazazi wangu yatakwenda kinyume na jinsi anavyotaka Mungu, nafaa kuyafuata nani?


Biblia inatwambia kuwa mamlaka yote inatoka kwa Mungu; Kulingana na jambo hili tunaweza kufanya jinsi wanavyotwambia wazazi wetu, huku tukizingatia kuwa hatufanyi jambo ambalo tunajua linamkasirisha

Mungu. Iwapo wazazi wetu wanatukataza kwenda kanisani, kuna machaguo ya kuweza kusikia kutoka kwa Mungu. Wakati utakuja ambapo maamuzi yatakuwa yetu, basi tunafaa kuwaheshimu wazazi wetu na kufuata amri za Mungu. Yote yanaweza kufanywa pamoja.

## MAJIBU YA MAFUMBO










## MCHEZO

***Kumbatiano za kimziki***

Panga kikundi kibinafsi au katika jozi hadi uunde kikundi kikubwa. Wakati muziki utaacha kuchezwa, kila mshiriki anampatia mwenzake kumbatio na kusema jina lao.
Muziki unaendelea na wakati mwingine unapowacha kucheza, watoto watatu wanawacha kucheza na kukumbatiana na kusema majina yao kwa namna hii hadi wajipate katika kumbatio kubwa la kimziki.







## KAZI YA ZIADA

Fikiria mambo ambayo umemwomba Mungu na umeyapokea wiki hii na iwapo Amekujibu kuhusu kitu chochote ambacho ulimwomba, aidha katika familia yako au katika maisha yako, chukua wakati na kumshukuru Mungu, halafu umwambie mwalimu kuhusu jambo hili katika shule ya Jumapili ya watoto.

# KUWA MNYENYEKEVU KAMA YESU 05



## Yesu aliiosha miguu ya mitume wake: Yohana 13:3-17

### SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Leo wanahitaji kuosha mashine baada ya misheni. Ajenti ameiosha mashine mara mbili mfululizo, na leo ni zamu ya mkaguzi. Hataki kufanya jambo hili na anajaribu kuepuka jukumu hili. Zaidi, yeyé ni mwanamemba mkuu katika timu, kwa hivyo Ajenti anafaa kuiosha tena. Kiongozi anamwambia kuwa leo ni zamu yake na anafaa kuiosha watakaporudi. Anakubali.

### SOMO

Yesu alikuwa akikula chajio na watume wake ambapo alifanya jambo lililowashtua sana mitume hadi Petero akamwambie awache.

Soma Yohana 13:3-17.

Kitu ambacho Yesu alifanya ni kile watumishi pekee wanakifanya. Katika Luka 22:27, Yesu aliwauliza ni nani aliye na hadhi, anayetumikia au anayetumikiwa. Hakika, ni anayetumikiwa. Ila Yesu alisema, “Niko kati yenu kama mtu anayewatumikia,” na alidhihirisha hili kwa Matendo yake. Hata aliosha miguu ya mtume ambaye alijua kuwa angemsaliti.

Yesu alionyesha unyenyekevu wake kwa watu wengine pia. Alikuwa tayari kutoka mbinguni na kuja hapa duniani kama mtoto! Hakuwa na makao wala maakazi yake kama mtu mzima wa kawaida. Hakuwa na watumishi. Hakuwashurutisha watu kumwabudu. Alipokuwa akihukumiwa, hakujibu kwa lawama za uongo. Hakuwakemea wanajeshi waliomcheka.

Na mwisho, Alikufa kwa ajili yetu, Kondoo wake. Wafilipi 2:8 inasema; “Akiwa kama mtu, Alijinyenyekeza kwa kutii hadi kifo chake, hata kifo katika msalaba.”

Yesu alisema kuwa tunafaa kufuata Mfano wake na kuwa mtumishi kwa watu wote. Sio tu wale ambao tunawapenda, ila watu wote ambao Mungu aliwaumba.

### AYA YA KUMBUKUMBU

*Wafilipi 2:3-4 "Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. 4Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine."*

### SARAKASI (SEHEMU YA 2)

Wanaporudi kutoka kwa ziara, wanajadiliana jinsi Yesu, ambaye ni mfalme katika ulimwengu, alipiga magoti na kuiosha miguu ya watume wake. Ilikaa kama kazi duni! Baadhi ya watume walikuwa na vipele katika vidole vyao vikubwa vilivyo na nywele! Na miguu yote ilinuka. Mchunguzi anaomba msamaha kwa mtazamo wake kuhusu kuiosha mashine. Kiongozi anafikiria kwa sekunde, halafu anasema kuwa ataiosha mashine leo, na

mchunguzi anaweza kuiosha wakati ujao. Kiongozi anafikiria kwa sekunde, halafu anasema kuwa ataiosha mashine leo, na Mkaguzi anaweza akaiosha wakati ujao. Mchunguzi anajitolea kuiosha dawati ya udhibiti wa oparesheni, na Ajenti anajitolea kuosha grisi kutoka kwa vipuri katika eneo la kiufundi.

## HAKI

Yesu alikuja kuwatumikia watu na sisi sote tunafuata mfano wake. Hivyo, tunafaa kila wakati kutafuta njia rahisi za kuwatumikia wengine, hata wale ambao walituumiza.

## WASIFU (MJUMBE)

Mjumbe ni mtu ambaye kazi yake ni kufanya huduma ya kuokota nyenzo za mawasiliano au vifurushi kutoka kwa yoyote ambaye anavihitaji na kisha kivichukua na kuvipeleka hadi mahali vimetumwa. Inaweza kuwa ni katika jiji moja au kati ya majiji tofauti.

Majukumu: Mjumbe anapaswa kuwa mwaminifu na anayetekeleza majukumu kwa namna iliyo salama. Ni muhimu kupata imani ya wateja wake ili akuze mtandao wa watu wanaowasiliana na hivyo kuwa na kazi nyingi.

Fursa: Wanapopata uaminifu, wanawabadilisha kwa namna iliyo ya kibinafsi, ambayo itakumbukwa kila mara. Tumia jambo hili ili kutoa huduma iliyo na jukumu, kila mara kufanya kila uwezalo katika kila upelekaji unaoufanya.

Hivi sasa, uaminifu kwa watu umepotea. Kwa sababu ya hali nyingi ambazo ni za utapeli au ulaghai ni ngumu kwa mtu kuacha kuwa na wasiwasi anapotumia huduma za ujumbe mara ya kwanza. Mjumbe anaamua iwapo hali hii inaendelea au itabadilika.

## MASWALI NA MAJIBU

1. Je, nafaa kufanya nini ili kuwa mnyenyekevu?

Ni katika hali nyingi ambapo tunaweza “kufanya mazoezi” ya kuwa wanyenyekevu. Tuko na fursa ya kuchagua kitu, na kuwa wanyenyekevu katika matendo yetu. Kuwafikiria wengine kujuliko na namna nyingine. Angazia kila tendo katika siku iliyopita na utaweza kuelewa iwapo unafaa kuwa na kiburi au iwapo unafaa kuwa mnyenyekevu.

2. Je, nafaa kupigania sifa zangu watu wanaposema uongo kunihusu?

Ni ngumu sana kuwa katika hali hii. Kwa kawaida huwa tunajitetea na kukataa kinachosemwa kutuhusu. Tunapoona alichopitia Yesu wakati wa majaribio, walimshtumu kwa mambo ambayo hakuyafanya ili wamuue. Ila hakusema lolote. Wakubalishe watu kuwa na muda wa kutambua kuwa mambo wanayoyasema kukuhusu ni ya uongo, bila kuzungumza nao kuhusu jambo hili na utaona mitazamo mizuri ya watu wako.


3. Je, nawezaje kuwafunza marafiki zangu kuwa wanyenyekevu?

Kitu kizuri unachoweza kufanya ni kuwaonyesha unyenyekevu ndani yetu. Maneno yanaweza kutafsiriwa visivyofaa; ila matendo yetu yanajiongelelea. Kuwathamini wale ambao wako na uwezo katika jambo na kuomba usaidizi ni tendo la unyenyekevu. Ishi kulingana na unachokijua.

## MAJIBU YA MAFUMBO





## MCHEZO

***Kijisanduku cha Mshangao***

Tayarisha kijisanduku au mfuko ulio na mfululizo wa kanda kadhaa za karatasi ambapo majukumu kadhaa yameandikwa. Kwa mfano, sema aya ya Biblia, imba wimbo, mpatie mtu mwingi krayoni zako, mpatie mtu mwingine kifaa chako cha kuchezea, miongoni mwa mambo mengine. Washiriki wataunda mduara watapitisha kijisanduku kutoka kwa mkono mmoja hadi mwingine hadi kutolewa kwa ishara fulani. Mtu aliye na kijisanduku wakati ishara inapotolewa anafaa kutoa kanda za karatasi na kufanya jukumu lililoandikwa. Mchezo utaendelea hadi karatasi zikwishe. Mshiriki ambaye anatenda shughuli ya mwisho sasa ataongoza mchezo.






## KAZI YA ZIADA

Saidia mtu kufanya kazi za nyumbani katika nyumbani kwako au shuleni, bila wao kukuomba uwasaidie na kazi hizi. Ukiwa shuleni, saidia kwa kuokota takataka kutoka kwa chumba fulani ambacho hujawahi kusafisha.

# ENYE UPENDO KAMA YESU 06



**Yesu alipindua meza: Marko 11:15-17 (Yohana 2:13-17)**

## SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Ajenti anaiambia timu kuwa anapanga fursa ndogo ya kibiashara na dadake. Yeye ni msanii anaweza kutengeneza pambo nzuri sana za ukuta, na baadhi ya mapambo aliyoyatengeneza yako na aya za Biblia. Anapanga kuyauza. Siku nyingine, aliona mtu akiuza bidhaa za kidini kwa bei ghali zaidi kwa sababu ni za kidini na hivyo zinafaa kuwaleta watu karibu na Mungu. Anapanga kupandisha bei ya mapambo ya kutundikwa kwenye ukuta yaliyo na aya za Biblia. Mkaguzi anasema kuwa sio wazo nzuri kupandisha bei. Ila Ajenti anasema kuwa hajakubaliana huku wakirudi nyuma katika wakati.

## SOMO

Yesu aliingia Yerusalemu akiwa amebebwa na punda na watu walimfuata wakiimba nyimbo za Kumtukuza na kuweka mavazi yao chini mbele yake. Hii ilikuwa ni ishara kuwa Yeye alikuwa ni Mfalme! Wayahudi walikuwa wakifanya vyema. Ila Yesu alipotembelea hekalu, aliwapata watu wakifanya biashara badala ya kuomba na kumwabudu Mungu, na makasisi walikubalisha jambo hili!
Soma Marko 11:15-17.
Jambo hili linaonekana kama tendo lililojaa hasira kutoka kwa mwalimu ambaye amekuwa akifunza upendo na unyenyekevu. Ila kuna jambo zaidi katika hadithi hapa. Sheria ya Agano la Kale ilimhitaji mtu kwenda katika hekalu mara moja kila mwaka na kutoa dhabihu ya vitu ambavyo walikuwa wamevuna au kulea. Iwapo ilikuwa ngumu kwa mtu kupeleka dhabihu aliyoitaka, wangenunua kitu Yerusalemu ili kutoa badala yake. Wafanyabiashara walikuwa wameunda duka ndani ya hekalu ili kuuza bidhaa hizi. Kwa bahati mbaya, walikuwa wakiuza bidhaa hizi kwa bei ghali sana kwa sababu ingekuwa ni ngumu kwa wasafiri kuvinunua katika maeneo mengine. Walikuwa wakiwatumia visivyofaa watu ndani ya hekalu ya Mungu! Hili lilimfanya Yesu kuwaita wezi!
Hakuna kitu kinamchokasirisha Mungu zaidi ya mtu anayeingilia kati ya wengine kumpata Mungu, kwa sababu anawapenda watu na anataka wawe Naye. Katika Mathayo 23:13, Yesu aliwakemea viongozi wa kidini kwa kuwaweka watu nje ya mbinginu. Wacha tujaribu kutoingiliana na njia ya mtu mwingine ya kumpata Mungu kwa kumwekea sheria au kwa kuwatumia ila tunafaa kuifanya kuwa rahisi kwake kumpata Mungu.

## AYA YA KUMBUKUMBU

*Mathayo 23:13 "Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnawafungia watu ufalme wa mbinguni; ninyi wenyewe hamwingii, wala wanaoingia hamwaachi waingie."*

## SARAKASI (SEHEMU YA 2)

Kurudi kutoka Yerusalemu katika siku za Yesu, Ajenti anashtushwa sana na tendo la Yesu kwa wafanyabiashara katika hekalu. Ajenti anamwuliza Kiongozi, anayemwambia kuwa Mungu anatutaka

tuwasaidie watu kumpata, ila sio kuwasukuma mbali au kuwatumia vibaya wanapojaribu kumtafuta Mungu. Baada ya kujadiliana mambo haya kwa dakika kadhaa, Kiongozi anamsaidia Ajenti kubadilisha mtazamo wake kutoka kwa kupata faida na badala yake kuitizima biashara yake kama fursa ya kuwasaidia watu kumpata Yesu. Anaamua kupunguza bei ya mapambo yaliyo na aya za Biblia na kumwuliza dada yake kumwuzia mapambo hata zaidi.

## HAKI

Yesu alitenda kwa hasira kwa wale waliokuwa wakiwatumia vibaya maskini kwa Jina la Mungu. Tunafaa kuwatetea wale ambao hawawezi kujitetea, hasa katika kanisa.


## WASIFU (MWANAJESHI)

Mwanajeshi, katika maana ya jumla, ni mtu ambaye amejitolea au yuko katika kazi ya uanajeshi kwa lazima katika kazi ya uanajeshi katika taifa. Mwanajeshi huyu anapokea mafunzo na vifaa vya kuilinda nchi yake na masilahi ya nchi yake.

Majukumu: Katika jeshi, vikundi vya wanajeshi vimetengwa katika huduma tofauti. Kwa mfano, wanajeshi wanaotembea kwa miguu, wanajeshi wa silaha, na wanajeshi wa kudumisha sheria na amani, n.k. Mwanajeshi anajua yuko na jukumu kubwa la utiifu, ushirikiano, na kuwa na busara.

Fursa: Mwanajeshi wa Kikiristo yuko na fursa ya kuwa mwaminifu, mwenye bidii, na anayefuata maagizo. Usitete na kuanza au kuueneza uvumi, kwa kujua kuwa tabia nzuri huwa zinafanya kikosi chako kuwa bora zaidi na kinachofaa kuheshimiwa. Mwanajeshi pia anaweza kutafuta njia za kuwasaidia wengine, kuwahimiza, na kushirikiana nao kama timu. Unaweza kusababisha mabadiliko makubwa katika kitengo chako, haijalishi cheo chako.

## MASWALI NA MAJIBU



1. Je, na iwapo ninavienzi vitu vyangu, ila sio kuhusu kumtumkia Mungu?

Inafurahisha sana jinsi tunavyovienzi vitu ambavyo tunavipenda. Iwapo tutamtumikia Mungu, inamaanisha kuwa tunaijua nafasi yake katika maisha yetu. Tukiwa sehemu ya timu ya spoti, au shughuli nyinginezo, tunatenga wakati wa kujitayarisha na kuhudhuria kila mkutano. Mungu akiwa na nafasi ya kwanza katika mambo tunayoyafanya, inakuwa rahisi kutenga wakati wa kutosha ili kuyafanya mambo haya, na bila shaka, kuyafanya kwa kujitolea, na kufurahia tunachokifanya.

2. Mara nyingine nahisi ni kwamba najidanganya na sipendi hisia hii ...

Kumbuka kuwa, unaweza kumwomba Mungu msaada katika hisia hii unapomfanyia kitu. Wavulana na wasichana wengi wanastarehevu katika makanisa yao ambayo hayana uchu kwa Mungu. Katika maeneo mengine ya dunia watu wengi wanaokoka. Wako na juhudi za kweli kwa Mungu. Nakualika kujitolea hisia ya kutokuwa mstarehevu na kumwomba Mungu kukupa juhudi za kweli unapomhudumia.

3. Je, nafaa kuiga hasira ya Yesu katika kuwatoa wafanyabiashara katika hekalu?

Mara nyingine, tunaangazia tu matendo ambayo yanaweza kutupatia fursa ya kufanya mambo ambayo tunataka kufanya. Katika wakati huu, Yesu alihisi hasira kwa sababu kumwabudu Mungu baba hakukupatiwa maana inayofaa. Hasira yake ilielekezwa kwa wafarisayo na walimu wa Sheria kwa sababu ya mambo waliyoyakubalisha katika hekalu. Inawezekana Mungu hatataka tufanye jambo ambalo ni kali. Tahadhari usifanye mambo ambayo yatawaumiza wengine, kwa sababu wao ni muhimu kwa Mungu.

## MAJIBU YA MAPAMBO

### FUMBO LA KUTAFUTA MANENO

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| O | U | B | I | A | S | H | A | R | A | H | U | B |
| Y | Y | Y | I | S | A | E | A | Y | M | V | H | D |
| A | M | E | G | M | F | A | L | M | E | M | A | W |
| S | F | R | R | H | D | U | I | K | I | S | B | P |
| I | K | U | K | U | A | V | E | M | O | M | U | A |
| R | U | U | N | M | S | Y | H | D | E | N | D | Z |
| A | A | E | I | Z | N | A | N | V | D | V | U | U |
| F | W | Z | D | E | A | E | L | A | G | H | A | K |
| A | E | H | Y | L | P | I | H | E | K | A | L | U |
| W | M | N | G | U | R | A | M | B | M | O | B | T |
| T | U | K | H | D | H | A | B | I | H | U | M | H |








## MCHEZO

***Ilete kwangu***

Washiriki watajigawanya katika timu ndogo na timu hizi zitakaa mbali na mwezeshaji iwezekanavyo. Mwezeshaji anasema, "Nilitee …" na kusema jina la kifaa ambacho kiko karibu. Kwa mfano, "Niletee viatu vya mwanamume au mwanamke" (vitu vinaweza kuwa vifaa ndani ya darasa.) Timu inakimbia kuleta kilichoitishwa. Unaweza kurudia mara kadhaa, na kuuliza timu kuleta vifaa tofauti.






## KAZI YA ZIADA

Unda orodha ya vitu au watu ambao unawapenda kumliko Mungu na ambao wanakufanya kukosa uchu kwa Mungu (rafiki msichana au mvulana, kazi ya shuleni, simu, spoti, vifaa vya kuchezea, marafiki). Mwombe Mungu kukufunza kuona njia Zake. Zaidi, tenga wakati zaidi wa kuzungumza na Mungu wiki hii.

# MOYO WA YESU KUFICHULIWA 07



**Shamba la Gethsemane: Mathayo 26:36-39, 47-54**

## SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Mchunguzi yuko na hofu sana leo. Jana alipata kuwa rafiki wa karibu, ambaye hivi juzi amekuwa akitumia wakati mwingi na msichana mwingine, alimsaliti mchunguzi na kumwambia msichana huyo mwingine mambo mabaya kumhusu, ikiwa ni pamoja, na moja ya siri zake. Mchunguzi alipata kujua hili kwa sababu msichana huyo mwingine hakuweka siri na sasa shule yote inajua kuhusu jambo hili. Halafu mwalimu aliwapa wote wawili mradi na kuwaweka pamoja na msichana yule! Kiongozi na Ajenti wako na hofu wakiwa na Mchunguzi na kujaribu kumtia moyo msichana Yule.

## SOMO

Soma Mathayo 26:36-39, 47-54.

Yesu aliingiwa na hofu kwa sababu alijua kuwa mambo mabaya yangemtendekea katika masaa yaliyofuata. Kwanza, Yesu alimtafuta Mungu katika maombi. Huu ni mfano mzuri wa tunalofaa kufanya tunapoingiwa na hofu au wasiwasi mkubwa! Tunaweza pia kufuata mfano Wake nyakati za uchungu kwa kumwomba Mungu kubadilisha mambo huku tukifuata wosia Wake, tukiwa na imani kuwa Mungu anafikiria uzuri kuhusu maisha yetu ya milele na pia walio karibu nasi.

Halafu Judasi, mojawapo ya wale ambao Yesu alikuwa amewachagua kuwa marafiki wa karibu, aliwaleta watu ambao walitaka kumdhuru Yesu moja kwa moja. Huu ulikuwa ni usaliti wa hali kubwa na inawezekana ulimtia Yesu hofu zaidi ya hofu aliyokuwa nayo.

Ila hata katika wakati huu mbaya, Yesu bado alimwita Judasi "Rafiki" na wakati mmoja wa wanaume waliokuja kumdhuru Yesu alipoumia katika vita, Yesu alihisi neema ya kusitisha ile vita na kumponya Yule mwanamume. Hadithi hii inaonyesha upendo wa Mungu kwa wazi. Wakati wa uchungu mkubwa kwa Yesu, bado aliweza kutenda kwa wema na kuonyesha upendo mkubwa kwetu sote, na hata kwa wale ambao walikua wakajaribu kumdhuru.

## AYA YA KUMBUKUMBU

*Luka 6:27 " Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, Wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi"*

## SARAKASI (SEHEMU YA 2)

Wanaporudi, wanashangazwa wanapojadiliana kuhusu walichokiona, na jinsi Yesu alivyowaonyesha wema wale ambao walikuwa wakijaribu kumtia mbaroni. Mchunguzi anaifikiria hali yake na msichana Yule shuleni na kutambua kuwa mambo haya yanafanana. Anaiambia timu kuhusu majibu yasiyokuwa sahihi katika kazi ya ziada ya msichana yule na hataki kumsaidia, anataka afeli. Ila sasa anatambua kuwa anafaa kumsaidia

msichana yule na kazi yake hata ingawa alimwumiza Mchunguzi. Ilikuwa ni ngumu sana, jambo ambalo linamfanya kushtushwa na tendo la Mungu. Timu inaamua kuomba pamoja na kumwomba Mungu kumsaidia Mchunguzi kuwa na wema kwa msichana yule, kujua kuwa anaweza kufanya hata yasiyowezekana kwa usaidizi wa Mungu.

## HAKI


Je, ushawahi kujua kuwa rafiki mmoja alisema kitu kisichofaa kukuhusu kwa watu wengine? Hili linahisi kama usaliti kwa sababu ni kweli ni usaliti! Tunafaa kujifunza kusema mambo mema kuwahusu watu wengine kila mara.

## WASIFU (MTAALAMU WA VIUNGO)

Mtaalamu wa matibabu ya viungo ni mtaalamu wa afya anayetambua, kuzuia na kutibu hali tofauti za maradhi (dalili fulani zinazohusishwa na magonjwa au msogeo fulani) ambaye ana lengo la uendelezaji na upataji nafuu wa viungo vinavyoathiriwa na uchungu bila kuhitaji matibabu ya dawa.

Majukumu: Kama daktari au mwuguzi, wanafaa kujitolea na kuwa na huruma nyingi kwa wagonjwa. Mtaalamu wa matibabu ya viungo sio anayekanda misuli, ila amepokea mafunzo ya chuo kikuu na anatibu magonjwa na kuyazuia kwa kutumia mbinu kama vile joto, baridi au matibabu ya maji au matibabu ya ukarabati wa kimwili.

Fursa: Mtaalamu wa matibabu ya viungo ambaye ni mkiristo anaweza kuwatia moyo wagonjwa, kufanya kazi na madaktari na wafanyakazi wengine, na kwenda sambamba na matibabu na mitindo ya kisasa. Kwa sababu mtaalamu wa matibabu ya viungo anawasiliana na wagonjwa wengi wakati wanapohitaji msaada, kuna fursa kubwa za ushauri rahisi na kusaidia katika familia na marafiki.



## MASWALI NA MAJIBU

1. Je, Mungu anaweza kuniokoa kutoka kwa mambo mabaya?

Bila shaka, Mungu anatutakia mema; Sisi sote tunapitia hali tofauti na mara nyingine “ni mambo mabaya” na yanaweza kutendeka ili kukakamilisha mapenzi ya Mungu katika maisha yetu. Tunapopitia hali mbaya, inaweza kuwa ngumu kuelewa ni kwa nini linafanyika. Tunapojiuliza ni “kwa nini” tumepoteza mwelekeo wetu. Mambo mazuri na mabaya huwa yanafanyika uliwenguni. Hata Yesu hangeepuka mateso kabla ya kusulubishwa. Ni lazima angepitia mateso ili kuingia katika hatua nyingine ya harakati zake. Ni sawa nasi kuwa, pia sisi, tunaweza kufanya hatua katika maisha ambayo Mungu anatutaka kuishi.

2. Ni ngumu kusamehe usaliti. Je, tunawezaje kusamehe usaliti?

Inalingana na kila mtu jinsi usaliti utakavyotuathiri, Yesu aliteseka kwa sababu ya kusalitiwa na mtu aliyekuwa rafiki yake; mtu aliyekuwa karibu naye kila mara. Ila wakati wa usaliti, hakuwa na hasira wala hakumkasirikia Judasi. Alijua kuwa matokeo ya hali hii yalikuwa kwa manufaa yetu sisi wote. Yesu alijua ni nini kilichokuwa katika roho za watu. (Yohana 2:26) Hili lingekuwa ni pamoja na usalaiti. Tunafaa kujua hili, pia, na kuwa inawezekana kumsamehe msaliti pia.

3. Je, naweza aje kuiponya roho yangu?


Tunaweza, ila ni ngumu kuiponya roho yetu iwapo imevunjwa mara mingi sana. Matendo tunayoyafanya au kuacha kuyafanya yanaweza kutuonyesha jinsi roho zetu ziko. Wakati Yesu alisalitiwa, ni wazi alihisi kuvunjwa moyo, ila katika wakati huu alinyenyekea na kumhurumia mmoja wa walinzi ambao walikuwa wakimkamata. Alirudisha na kuponya sikio ambalo Pedro alikuwa amelikata. Siko hakika iwapo tungetenda kwa namna hii. Yesu alituonyesha kwa tendo hili lake kuwa roho yake haikuwa imebadilika.

## MAJIBU YA MAPAMBO



FUMBO LA KUTAFUTA MANENO

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| J | L | K | D | U | W | G | M | T | U | J | I | A | G | A | T |
| S | U | H | I | A | R | I | M | A | E | H | F | L | T | U | A |
| H | M | D | A | Y | R | P | T | A | O | Y | A | O | F | G | M |
| I | U | I | A | E | I | E | O | G | A | I | M | I | M | T | B |
| W | K | A | G | S | W | I | M | N | E | D | B | M | N | S | U |
| S | R | I | H | U | I | M | J | S | Y | I | U | G | M | I | A |
| T | O | A | F | Y | F | E | M | H | R | A | L | I | O | E | R |
| A | H | S | I | A | M | A | W | A | D | U | M | A | W | K | U |
| F | O | M | H | A | R | L | H | K | M | L | S | E | A | N | I |
| A | K | M | L | U | Z | U | R | I | Z | A | W | U | G | L | I |



**Jibu maswali kulingana na unachokiamini.**


1. Je, jina la rafiki yako wa karibu ni gani? *Jasmine*
2. Je, unaweza kufanya nini iwapo rafiki yako wa karibu atakusaliti? *Niko na hofu sana* *Nahisi nimesalitiwa na nimedanganywa.*
3. Je,unaweza kufanya nini rafiki yako akakuuza kwa ajili ya pesa au kusema siri kubwa kukuhusu?
4. Je, unadhani ni kwa nini Yesu aliponya sikio la mwanajeshi ule? *Kwa sababu licha ya hata haya yote, Yesu aliwaonyesha watu wote upendo na urafiki mkubwa.*
5. Je, unaweza kusamehe usaliti kama jinsi alivyofanya Yesu na kwa nini? *Bila shaka, kweli, Yesu amenisamehe. Je, mbona pia mimi nisijisamehe?*
6. Je, unafaa kuomba lini? *Katika wakati wowote, wakati ambapo mambo mazuri au mabaya yanapotutendekea.*



## MCHEZO

***Je, wewe ni nani?***

Mwambie mtu mmoja atakayejitolea kutoka nje ya chumba. Aliyejitolea akiwa nje, wengine wa washiriki watamchagulia ajira. Inaweza kuwa ni ajira ya mwigizaji kutoka kwa wasifu katika masomo ya darasani. Aliyejitolea atakaporudi, washiriki wengine wataiga shughuli za mtu huyu. Aliyejitolea ni lazima aige ajira ambayo imechaguliwa / kulingana na shughuli ambazo zinafanywa.







## KAZI YA ZIADA

Wiki hii iwapo mtu alikukosea kwa namna isiyofaa au kukukemea, usipigane naye. Tulia na umwombee na kumwomba Mungu kukupa amani. Zungumza na walimu wako wa Shule ye Upili ya watoto kuhusu jinsi ulivyohisi.

# UDHALIMU!

08



## Yesu ahukumiwa: Marko 14:57-65, 15:1-15

### SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Ajenti amekasirika leo. Anaiambia timu kuwa shule ilikuwa ikimlaumu kwa sababu ya mpira uliopotea. Ni hakika kuwa sio yeye aliyeuchukua! Alimsikia mtu akisema kuwa anafikiria ni yeye kwa sababu yeye ni Mkristo, jambo ambalo lilimkasirisha sana. Anajitetea kwa marafiki wake, Kiongozi na Mchunguzi. Kiongozi anamwamini na kumtuliza kabla ya wao kurudi katika wakati wa zamani.

### SOMO

Soma Marko 14:55-65, 15:1-15.

Yesu hakuwa na hatia. Hata uongo uliosemwa kumhusu haungeaminika. Yesu baadaye aliwasaidia waliokuwa wakimshtumu kwa kusema kuwa Yeye Alikuwa ndiye Mesiya. Viongozi wa kidini walihisi kuwa jambo hili lilitosha kumhukumia kifo. Kwa sababu hawakuwa na mamlaka ya kumwua mtu yeyote, walimtuma Yesu kwa Pilato, kiongozi wa Kirumi, ila Pilato hakumpata Yesu na makosa yoyote kisheria. Ila viongozi wa Wayahudi waliwashawishi watu kusema Yesu auawe.

Katika haya yote, Yesu hakujitetea. Labda, iwapo angezungumza ili kujitetea, hangeuliwa. Ila Yesu alijua kuwa ni lazima jambo hili lingetendeka ili tuokolewe.

Kumuadhibu mtu aliye na makosa ni sawa na pia si sawa. Ila, Yesu hakuwahi kufanya dhambi na bado aliadhibiwa kwa njia mbaya zaidi. Alijitolea kupitia udhalimu mkubwa sana katika wakati wa maisha yetu kwa ajili yetu!!

### AYA YA KUMBUKUMBU

*Isaya 53:9 "Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake."*

### SARAKASI (SEHEMU 2)

Wanaporudi, wanazungumza kuhusu Yesu akihukumiwa na jinsi ambavyo hakusema neno lolote ili kujitetea, ila aliwaachilia Kumhukumia kifo. Ajenti anasema kuwa jambo hili sio sawa. Kiongozi anamhimiza kuwa Mungu ambaye ana nguvu zaidi juu ya vitu vyote ataleta haki mwisho wa kila kitu. Wanasoma 1 Petero 2:23 na kuona jinsi Yesu alivyomwamini Mungu ambaye ana haki. Halafu wanasoma Wafilipi 2:5-11 na kuona jinsi Yesu anavyoinuliwa juu ya kila mtu mwishowe. Ajenti anahisi vyema sasa, kujua kuwa Mungu anaona kila kitu na kujua kuwa hakuuchukua ule mpira kutaleta haki mwishowe.

## HAKI

Je, ushawahi kushtumiwa kwa jambo ambalo hukulifanya? Ni uchungu mwingi. Ni lazima tumakinike tunapomshutumu mtu kwa jambo.


## WASIFU (JAJI)

Jaji ni mtu aliye na mamlaka ya juu zaidi katika korti ya haki. Wanatatua migogoro kati ya watu wawili, au kuamua maisha ya mtu anayeshtumiwa kosa kwa kuzingatia ushahidi uliotolewa katika kesi.

Majukumu: Ili kutoa haki, jaji yuko na maarifa mengi kuhusu sheria kwani wako na jukumu la kufuatilia ufuataji wa sheria. Jaji ni mtu na, hivyo, anaweza kufanya makosa katika uamuzi wake.

Fursa: Jaji mkiristo ako na fursa ya kutoa uamuzi na kusimamia watu wengi. Wanaweza kushawishi sio mfumo wa korti pekee, bali pia shughuli za polisi, shule, na taasisi za umma. Vitu hivi vyote ni muhimu kwa Mungu, ili aweze kufanya kazi yake nzuri jinsi inavyofaa huku jaji akizingatia kuwepo kwa Mungu.

## MASWALI NA MAJIBU



1. Je, kuwa mtu aliye na dini ni nini?

Inaaminisha watu wanaotaka kufuata maelezo ya Biblia moja kwa moja, kama katika hadithi hii; walitaka kutumia ujuzi wao katika kuwashtumu wengine, ila hawafuati amri za Mungu kama wanavyosema. Kwa kawaida, tunaweza fanya hivi, kuwataka wengine kufanya mambo ambayo sisi hatuwezi kuyafanya.

2. Je, mkoseaji anafaa kuadhibiwa?

Kama tunavyoona, kila mtu ambaye amefanya dhambi anafaa kuadhibiwa. Ila Yesu anaweza kubadilisha fikra zetu. Walipompeleka mwanamke mzinifu kwake, hakumshtumu hata ingawa alipatikana akifanya dhambi (Yohana 8:1-11). Yesu aliwaambia waliomshtumu, “Yoyote ambaye hajawahi kufanya dhambi, awe wa kwanza kutupa jiwe.” Hili linatuonyesha kuwa hatufai kuwawekea watu wengine sheria au kuwashtumu kwa sababu tunaweza kujipata katika hali kama ile ile.


3. Je, naweza kufanya nini iwapo nitahisi nimekosea kuhusu jambo fulani?

Tunapohisi kuwa hatujafanya jambo vinavyofaa, tunahisi tumekosea; Tunaweza kusema kuwa ni jambo nzuri kuhisi vibaya kwa sababu tunatambua kuwa tumekosea. Jambo linalofaa ni kujifunza kutokana na hali hii na kuweza kutenda kwa namna tofauti. Wakati mwingine jambo kama hili litakapotokea, tunafaa kuomba msamaha na kurekebisha makosa yetu. Soma 1 Yohana

## MAJIBU YA SHUGHULI






## MCHEZO

***Habari Habari***

Washiriki watasimama na kuunda mviringo. Mtu atatembea na kuzunguka mviringo huu, akiwa nje na kugusa bega la mtu. Huyu mtu atatembea kuzunguka mviringo huu katika upande tofauti, hadi wakutane uso kwa uso. Watasalimiana mara tatu kwa majina yao. Wawili hao watakimbia katika upande tofauti na kuuzunguka mviringo, hadi wajipate katika eneo wazi. Mtu atakayeshindwa atatembea na kuzunguka mduara huu tena na mchezo utaendelea hadi kila mtu akuwe na fursa yake.






## KAZI YA ZAIDA

Iwapo katika wiki hii mtu alikushtumu kwa sababu ya makosa sio yako, usijitetee. Mwombe Mungu kumfanya mtu yule kuona kuwa amefanya makosa na kukubali makosa yake. Iwapo hatakubali makosa yake, mwache Mungu kulifanya katika wakati unaofaa.

# KUISHI KATIKA KIFO

09



**Yesu Asulubiwa: Mathayo 27:27-31, 45-54**

## SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Ajenti anaingia na jibu. Anang'ang'ana kuipunguza hasira yake, mara nyingi anamkemea kwa sauti kubwa dadake anapomdhihaki. Na ako na wasiwasi kwa sababu alisahau iwapo aliomba wokovu au iwapo aliomba maombi yanayofaa. Je, Mungu alimsikia? Je, na iwapo atamkemea dadake kwa sauti kubwa na kitu kimfanyikie dadake kabla yake kuomba msamaha? Kiongozi anamtia moyo, huku akisema kuwa anakumbuka Ajenti alipomkubali Yesu na kwamba Yesu alimwokoa kwa kuondoa dhambi zake za zamani na za siku zijazo. Ajenti hajashawishika kabisa wanaporudi katika wakati wa zamani Yesu akisulubiwa.

## SOMO

Wanajeshi walimchekelea Yesu na kumpiga na kumpigilia misumari msalabani. Yesu alipitia kifo cha polepole, kilichokuwa na uchungu, na kibaya sana msalabani. Hili lilikuwa jambo mbaya. Ila hili lilikuwa tukio lililokuwa na nguvu sana hata ulimwengu ulitingika! Hata viongozi ambao hawakuwa wa kidini walitambua kuwa tukio hili lilikuwa jambo muhimu la kiroho na kusema kuwa ni kweli Yesu alikuwa ni mwana wa Mungu. Pazia lililokuwa limetenganisha eneo Patakatifu pa Patakatifu iliraruka, kuonyesha kuwa sasa tunaweza kuwasiliana moja kwa moja na Mungu baba! Dhambi zetu sasa huwa haziingii kati yetu na Mungu kwa sababu anatupatia wema wake kama zawadi ya bure. Hatuwachwi nje ila sasa tunaweza tukaungana na familia Yake kama wana wa kiume na kike walio na hadhi kwa muda wa milele. Na sasa hatufai kuogopa kifo au adui au kitu chochote kwa sababu ameshinda kifo kabisa na anatuwezesha kupata mamlaka na uwezo Wake.

Kitabu cha Waebrania kinaonyesha wazi kuwa hata viongozi wakubwa wa kidini ambao walikuwepo kabla ya Yesu na walitazamwa kama wasio na dhambi hawakufaa kutazamwa hivyo ila waliokolewa na alijokifanya Yesu. Hili ni jambo la kujitolea sana katika wakati wote na Yesu alitufanyia jambo hili! Tunawezaje kufanya jambo lolote ila kukubali zawadi kuwa Yesu alitufia msalabani na kumkubali Yesu kama Mungu na Mwokozi!

## AYA YA KUMBUKUMBU

*Isaya 53:5 "Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona."*

## SARAKASI (SEHEMU YA 2)

Kurudi kutoka siku za zamani, timu bado inashtuliwa na ilichokiona. Wanazungumza kuhusu uchungu alioupitia Yesu, na jinsi ambavyo alipigwa na walinzi. Halafu wanazungumza kumhusu aliposulubiwa na giza kubwa lililojaa kila mahali. Halafu ajenti anawaambia alichokisema Yesu, "Imemalizika" (Yohana 19:30) na jinsi ambavyo Ajenti alijua mara moja kuwa Yesu alikuwa akizungumzia dhambi zote za Ajenti alivyosema hivyo! Ajenti anaruka ruka huku akisema, "imemalizika!" Wakati huohuo, Kiongozi na Mchunguzi wanazungumza kuhusu mtetemeko wa ardhi na mawe kuvunjika na kelele watu waliokufa walipofufuka.

## HAKI

Jambo la ukarimu mkubwa, ambalo tunaweza kuwafanyia watu ni kuwaambia kuhusu hadithi ya Yesu na jinsi Alivyotufia ili tuweze kuishi!


## WASIFU (MLINZI)

Mlinzi ni jina linalopatiwa mtu ambaye anatoa huduma za ulinzi. Inafaa kutajwa kuwa ni kazi iliyo na masaa ambayo hayabadiliki na mara nyingi inachosha sana. Katika aina fulani za biashara na ajira, mtu anayefanya kazi hadi masaa ya ziada anajulikana kama mlinzi.

Majukukumu: Kwa kawaida, kampuni huwa ziko na mlinzi wakati wa masaa ya ofisi, na mwingine wakati ofisi imefungwa. Huyo wa pili ni lazima awe hapo wakati mrefu, kwa kawaida peke yake, huku akisikiza kelele yoyote, na msogeo wowote usio wa kawaida.

Fursa: Mlinzi Mkristo ako na fursa ya kuwatunza watu na raslimali za kampuni. Mlinzi huyu anaweza kuwatendea watu kwa wema ila ajue kuwa anaweza kushinikizwa kufanya mambo zaidi ambayo hayafai kufanywa. Uadilifu sanasana ni kitu cha muhimu. Kuwa mwema, ila usimwamini kila mtu huku ukihakikisha unafuata maagizo na maazimio yote ya kazi yako.

## MASWALI NA MAJIBU




1. Je, sisi wote ni wana wa Mungu?


La, jambo la kweli ni kuwa sisi wote ni viumbe wake. Neno hili limechanganywa. Ili kuwa mwana wa Mungu, tunafaa kukubali Yesu Kristo kama Mwokozi na Mungu wetu. Soma "Yohana 1:12" Kwa kumpa Mungu mioyo na maisha yetu, tuko na haki ya kuitwa watoto wake, hakuna njia nyingine.


2. Je, ni kwa nini Yesu alitukufia?

Kwa sababu anakupenda. Katika tendo la upendo ambalo sisi hatufai kulipokea, Soma Yohana 3:16 na utambue kuwa, "Kwa Maana Mungu aliupenda ulimwengu kiasi cha kumtoa mwana wake wa pekee aliyempenda sana, mwana wake; ili kwa kifo tuweze kuokolewa. Damu yake inazingira makosa yetu sote na kwa sababu ya jambo hili, Mungu anatuona kama watoto wake. Yesu aligeuka kuwa mwana wa pekee (mwana pekee wa Mungu): na kuwa mwana wa kwanza (anayepokea uridhi mkubwa). Ni dhabihu ambayo tunafaa kuikumbuka na kupenda, na ni kwa hivyo ni muhimu kuwaambia marafiki na familia yako.

## MAJIBU YA MAFUMBO







## MCHEZO

***Watu watatu***

Mwalimu anawagawanya wanafunzi katika timu tofauti zikiwa na wachezaji watatu katika kila timu, ambazo zinaunda mistari katika mstari wa kwanza. Mwalimu atakapotoa ishara, wale walio katika mstari wa kwanza watakimbia, kufikia goli, kurudi na wa pili anauchukua mkono wa mtu wa tatu. Watatu hao wanakimbia tena bila kuachiliana mikono wakati wowote kuelekea kwenye goli na kisha kurudi katika eneo la kuanzia. Timu inayomaliza ya kwanza ndiyo inayoshinda.






## KAZI YA ZIADA

Zungumza na wazazi wako au mtu yeyote ambaye unamwamini kuhusu jinsi ulivyohisi ulipojua alichokipitia Yesu aliposulubiwa na jinsi unavyohisi kuhusu zawadi ya wokovu aliyokupatia.

# MTU ASIYE NA MAANA KUOKOLEWA 10



**Mwizi katika Msalabani: Luka 23:32-33, 39-43**

## SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Mchunguzi ako na mtu wa familia aliyeishi mbali ambaye alifariki hivi majuzi. Ako na wasiwasi kuhusu mwanafamilia huyu kwa sababu hajakuwa akimfuata Mungu wakati huu wote, ila babake alimtembelea na kumwombea kabla yake kufariki. Hajui anachofaa kufikiria. Katika kujadiliana analofaaa kufanya, timu inaamua kurudi kwenda kuona kusulubishwa kwa Yesu kwa sababu kuna mambo ya kuona katika wakati mfupi sana. Kiongozi alikuwa amesikia mazungumzo kiasi ambayo yalikuwa muhimu ila hakuyaskia yote wakati wa kwanza. Hata ingawa wazo la kumwona Yesu akiteswa tena linaonekana kuwa chungu, wanaamua kurudi tu na kujificha katika eneo jingine ambapo wanaweza kuskia hata vizuri zaidi.

## SOMO

Soma Luka 23:32, 33, 39-43

Yesu alipouliwa katika msalaba, wahalifu wawili pia waliuliwa pamoja naye. Yesu alizungumza na mmoja wao kwa ufupi. Mwanamume huyu alimwomba Yesu kumkumbuka. Yesu akamwambia kuwa angekuwa naye paradiso. Tena, tunamwona Yesu akichukua muda na nguvu ya kuzungumza na mtu hata ingawa alikuwa katika uchungu mwingi sana.

Hatujui ni uhalifu gani ambao yule mwizi alikuwa ameutenda ili kusulibiwa. Kwa namna kama hii, mambo yasiyofaa ambayo tumeyafanya hayajalishi kwa sababu dhabihu timamu ya Yesu iko na nguvu kuliko kitu chochote. Yesu alijitolea kufa ili sisi tuweze kuwa na maisha ya milele naye!

Huu ni ufafanuzi rahisi zaidi, ambao ni wa moja kwa moja jinsi gani tunaweza kuokolewa kutoka kwa dhambi zetu kupitia Yesu.

## AYA YA KUMBUKUMBU

*Warumi 10:11 " Kwa maana andiko lanena, Kila amwaminiye hatatahayarika."*

## SARAKASI (SEHEMU YA 2)

Baada ya kurudi, Mchunguzi anahisi faraja na anafurahia kuwa mtu kama mwizi aliyefariki na Yesu angeweza kuokolewa na kwamba Yesu angemkaribisha Paradiso hivyo tu. Timu inajadiliana jinsi kwamba, kama dhambi za Ajenti za zamani za siku zijazo zilivyoondolewa na damu ya Yesu msalabani, hivyo dhambi za maisha yote ya mwanafamilia wa Mkaguzi zimeondolewa na Yesu. Kwa uhakika, afadhali kuishi na Yesu katika maisha haya na kuhisi upendo na furaha Yake sasa badala ya kungoja hadi wakati wa mwisho. Ila wanahitimisha kuwa Yesu ana nguvu.

## HAKI

Jinsi tunavyoweza kuikubali zawadi ya Yesu, haijalishi tunapotoka au ambacho tumekifanya, watu wengine pia wanaweza kuipokea zawadi ya Mungu ya bure kwani haijalishi wanapotoka au waliyoyafanya.


## WASIFU (MWIMBAJI)

Mwimbaji ni mtu anayeimba kitaalamu na ambaye amesoma ili kupata ajira kama mwimbaji. Mwimbaji amejitolea kuimba, na bila shaka, anatumaini kupokea malipo kwa kufanya jambo hili.

Majukumu: Mwimbaji anafaa kujitolea kujifunza ustadi wake wa kuimba, kwa umakini mkubwa na mazoezi kwani hivi ndivyo mwimbaji anavyopata malipo. Iwapo mwimbaji atapata sifa za umaarufu, ni muhimu kila mara kumtukuza Mungu na kukumbuka kuwa kwa kutumia mziki tunaweza tiana moyo. 1 Wakorintho 14:26

Fursa: Waambaji wa Kikristo wako na jukumu sio tu la kuwa na ujuzi wa kimziki, ila pia kuwa na uhusiano wa undani na Mungu. Wanaweza kuwa vifaa vinavyotumiwa na Mungu, hasa wanapoongoza Kanisa katika kumtukuza Mungu.

Hivi sasa mitandao ya kijamii inaifanya kuwa rahisi kujitambulisha kama mwimbaji, na wengine wamepata umaarufu kwa namna hii. Mwimbaji anaweza kuhisi uwepo wa Mungu na kutumiwa na Mungu kuwasaidia wengine ili kuhisi uwepo wa Mungu pia.



## MASWALI NA MAJIBU

1. Je, naokolewa tu kwa kumkubali Yesu kama mwokozi wangu?


Ni rahisi kama hivyo. Inapofanyika kwa ukweli kabisa, utaonyesha na matendo yako kuwa yeye ni Mungu katika maisha yako. Matendo yanayokuonyesha kuwa umeokolewa ni tofauti na kila mtu, na mara nyingine mabadiliko yanafanyika polepole na mara nyingine yanaonekana mara moja. Na mara nyingine, mtu anamwomba Yesu kuwa mwokozi ili kupokea zawadi au manufaa kiasi, huu sio wokovu wa ukweli.


2. Je, ilikuwa ni haki kwa mwizi msalabani kuokolewa hata ingawa alikuwa mwenye dhambi?

Yesu alitambua mwizi alikuwa amejinyenyekeza na alimtetea Yesu. Jambo hili linaonyesha kuwa mwizi alikuwa ametubu, na Yesu zaidi ya watu wengine angeweza kujua kama alikuwa ametubu kwa kweli. Kumbuka kuwa, hatufanyi maamuzi jinsi wokovu unapaswa kuwa, badala yake, tunasoma Biblia ili kujifunza tunachoweza kufanya kuhusu wokovu huu.

## MAJIBU YA MAFUMBO






## MCHEZO

***Wa mwisho atakuwa wa kwanza***


Washiriki wote wasimame katika mstari wa kwanza na, mwalimu atakapotoa ishara, watoke "wakikimbia" kana kwamba wanachukuliwa filamu ya mwendo wa polepole. Wa mwisho kufikia goli ndiye mshindi.




## KAZI YA ZIADA

Unda orodha ya vitu ambavyo unamwania Mungu atakusaidia kusuluhisha. Zungumza na mtu mwingine kuhusu vitu hivi. Katika mwisho wa orodha weka andiko hili Warumi 10:11, "Na hivi yanasema maandiko: Yoyote amwaminiye hataibika kwamwe."





**Ufufuo wa Yesu: Mathayo 27:57-61, 28:1-10, Luka 24:36-48**



## SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Ajenti anakuja ameshtuka leo. Anaiuliza timu ni kwa nini Yesu alitufia? Halafu tunapata uhai katika maisha yetu ila Yeye ameshakufa? Kiongozi anamwambia kuwa Yesu bado yuko hai. Ajenti anajibu kwa kusema kuwa kweli ameshafariki kwa sababu walirudi katika wakati na kuona kufariki kwake mara mbili! Yesu anaweza kuwa aje hajafariki na tuliona kifo chake? Kiongozi anafurahia huku wakijitayarisha kurudi katika wakati wa zamani, ila anamtaka Ajenti kujionea yeye mwenyewe.

## SOMO

Soma Mathayo 27:57-61

Kwa waliomwamini Yesu, huu ulikuwa ndio Mwisho. Hata kusema walihisi kuvunjika moyo ni jambo ndogo. Ilikuaje kitu cha kuvunja moyo sana kwa waliomfuata Yesu. Waliamini kuwa Yesu alikuwa Mesiya ambaye watabiri wakubwa wa zamani walitabiri kuwa angekuja na kuikoa Isreali. Walikuwa wamewacha kazi na familia zao ili kumfuata Yesu. Na sasa, Yesu alikuwa amefariki na pia ndoto zake naye.

Ila Yesu hakukaa katika kifo kwa muda mrefu…

Soma Mathayo 28: 1-10 na Luka 24:36-48

Jambo la kufurahisha sana! Alichokisema Yesu ni kweli! Yesu alikuwa hai! Katika siku chache zilizofuata, Yesu alijionyesha kuwa hai kwa mamia ya watu. Walifurahia sana!

Mara nyingine tunafaa tu kumwona Yesu. Mambo yakiwa magumu, wacha tumwombe kujidhihirisha, halafu Tumtafute na pia Uwezo wake unaofanya kazi katika maisha yetu na katika maisha ya wanaoishi karibu nasi. Mara nyingine Yesu alikuwa ametabiri kifo na kufufuka kwake!! Alionyesha uwezo wake mkubwa, kuondoa shaka yote, tunaweza kumwamini na kumfuata katika maeneo yote ya maisha yetu.

## AYA YA KUMBUKUMBU

*Waebrania 11:1 " Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana."*

## SARAKASI (SEHEMU YA 2)

Wanaporudi, wako na furaha tele, hasa Ajenti ambaye hapo awali hakujua kuwa Yesu alifufuka kutoka kwa wafu! Wanajadiliana jinsi Yesu alivyo zikwa, halafu asabuhi wanawake walipokwenda na malaika… ila sehemu

inayowapendeza sana ilikuwa pale ambapo mwanamume alipowakaribia na mara moja, wakatambua huyu mwanamume alikuwa ni Yesu! Wanajadiliana jinsi ya kuingia chumbani haraka kabla ya kufungwa kwa chumba na watume wa Yesu, hii ni misheni inayohitaji ujanja mwingi kuliko zingine, halafu jinsi Yesu alivyotokea mara moja katika chumba! Ajenti kwa furaha anafikiria jambo hili linavyomaanisha na jinsi ambavyo atakuwa na mwili mpya kama Yesu alivyokuwa, unaoweza kujitokeza katika mahali tofauti na kula samaki, hata ingawa anagependa kuku. Anamwuliza Kiongozi anayemjibu kuwa hajui jinsi miili yetu itakuwa, ila itakuwa mizuri sana!

## HAKI


Kila mtu anakufa moyo mara nyingine. Wacha tuhisi hofu pamoja na marafiki zetu walio na hofu, ila tuwakumbushe kuwa Mungu wetu mzuri anayeleta mazuri kutoka kwa hata hali mbaya zaidi.

## WASIFU (MMISIONARI)

Mmisionari ni mtu ambaye ameitwa na Mungu na mara nyingine anaiwacha nchi yake na utamaduni wake na kwenda katika eneo jingine.

Wengine wanaamini kuwa mmisionari anawalazimisha watu kubadili dini yao, ni kwa sababu hii katika mataifa mengi ambapo wanaabudu Miungu mingine hawakubalishwi kuingia au walio tayari katika maeneo haya wananyanyaswa au hata kuuliwa.

Majukumu: Wanahitaji kufunzwa kabla ya kutumwa katika maeneo mapya, ili kujua jinsi watakavyoishi katika tamaduni mpya wanapotumikia, huku wakijifunza kula vyakula “nadra”, kuvaa mavazi tofauti, kujua na kujifunza lugha mpya ya eneo hili, ila juu ya yote kuchukua tahadhari wakisambaza neno la Mungu katika tamaduni uliyopo, ili milango ikae kama imefunguka. Na pia kupokea utunzaji kwa sababu ya hisia zako ukiwa nje ya taifa au mahali ulikotoka.



Fursa: Wanamisionari ni mifano ya imani ndani ya Mungu, na usaidizi wake katika nyakati gumu, na pia uwezo wa Mungu wa kuifungua milango na kubadilisha maisha na kuwa mwadilifu. Mmisionari ni mtu ambaye amejitolea katika jambo hili na mara nyingi huwa anafanya hivi kwa kujitolea kabisa, kujitolea Kimungu, na kupenda kufuata nyayo za Mungu na kuutimiza utume mkubwa.

## MASWALI NA MAJIBU

1. Je, inachosema Biblia bado ni kweli?

Neno la Mungu huwa halibadiliki, mambo yaliyosemwa miaka mingi kabla ya kuzaliwa kwa Yesu, yalitimia. Sasa tunaweza kuona ni kwa jinsi gani ahadi zilizoandikwa zinatimizika katika maisha yetu. Iwapo uko hata na imani ndogo, utaweza kuona ahadi zikitimizika. Soma Mathayo 24: 35 amini tu.


2. Je, ni kwa nini ni ngumu kwangu kuwa na imani kwa Mungu katika nyakati Ngumu?


Ni kawaida kuwa na shaka kuwa hatuwezi kuendelea. Katika nyakati ngumu, kwa mfano, babako anapopoteza kazi na uko karibu kurudi shuleni, au mamako anakuwa mgonjwa kwa kirusi kibaya kama cha Korona, itakuwa ni neno la Mungu lililopo katika kumbukumbu ya akili yako na pia katika roho yako ambazo zitakusaidia kuwa na imani.

Fikiria jinsi walivyohisi watume Yesu alipofariki msalabani. Yote waliyoyaamini, tumaini lao, matarajio yao pia yalikuwa yakikwisha, ilikuwa ni maneno ya Yesu ambayo yaliwasaidia kuendelea kuwa na imani.

## MAJIBU YA MAFUMBO










## MCHEZO

### *Wa Bluu na wekundu*

Mwalimu anaunda timu mbili zinazotoshana, moja ambayo ni ya "wekundu" na nyingine ambayo ni ya "bluu". Timu zote zimewekwa katika safu huku zikiangaliana. Mwalimu atakuwa ndiye anayepatiana amri. Kwa mfano, anaposema "wekundu" timu hii inafaa kukimbia hadi eneo lililokuwa limetengwa hapo awali nyuma yake. Iwapo mwekundu atamshika wa bluu, timu ya bluu itageuka kuwa nyekundu na kuungana na timu inayopinga. Timu itakayoweza kuingiza wachezaji wengi kutoka timu hiyo nyingine, basi itashinda.






## KAZI YA ZIADA

Wakati wa chajio, jadiliana na familia yako kuhusu wakati mzuri uliokuwa nao katika shughuli yoyote ya mkutano. Waambie ni kwa nini.

# MTU ASIYETARAJIWA AAMINI 12

**Saulo aamini: Matendo ya Mitume 9:1-20**



## SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Ajenti anakuja leo na kushindwa mbona Mungu aliamua kumwokoa? Hajatoka makaazi ya Wakiristo, na anajua mambo machache kuhusu Mungu. Anapohisi furaha, anashangaa kuwa Mungu anaweza kumwokoa na kumsaidia yeyé kati ya watu wote, hata ingawa alikuwa amefanya mambo mengi yasiyofaa hapo awali. Kiongozi anapendekeza kuwa wanafaa kurudi kumwangalia mtu ambaye haiwezekani kuwa Mungu alimwokoa. Wanarudi katika wakati ili kukutana na Saulo (Paulo).

## SOMO

Hata baada ya kumsulubisha Yesu, viongozi wa kidini walijaribu kuwafanya watu kukosa kumwamini Yesu. Mwanamume aliyeitwa Sauli ambaye alikuwa kiongozi aliyeiga uongozi wa kidini alidhani alikuwa akifanya alichotaka Mungu kwa kuwanyanyasa Wanakristo.
Soma Matendo ya Mitume 9:1-22.

Anania ni lazima alikuwa na imani kubwa ili kufuata mwongozo wa Yesu na kwenda kwa Sauli ambaye alikuwa akiwakandamiza Wakristo. Ila, angalia matokeo mazuri yaliyotokea! Saulo kumpata Yesu kuliyabadilisha sana maisha yake. Saulo (pia anaitwa Paulo) alibadilika kutoka kuwa mtu aliyekasirika na kuwadhulumu wengine na kuwa mtu aliyewaambia wengine kuhusu upendo wa Mungu. Alianza kufanya ziara katika ulimwengu wote na kuwaambia watu kuhusu Yesu. Alianza makanisa kadhaa na kuwa mmoja wa Wakiristo katika historia. Mungu alijawa sana na furaha kwa sababu ya Paulo hata Mungu alihifadhi baadhi ya mambo ambayo Paulo aliyasema katika Biblia.
Tunaweza kuwa kama Anania na pia kama Paulo, kuwaambia watu kuhusu Yesu na jinsi ya kumfuata. Tunaweza kukosa kuona katika ulimwengu jinsi Mungu anavyotenda kutupitia au kupitia watu tunaowaleta kwa Yesu, ila tukienda mbinguni tutashtuka na kujawa na furaha na kumtukuza Mungu tukipata alichotufanyia Mungu kupitia maisha yetu.

## AYA YA KUMBUKUMBU

*Matendo ya Mitume 1:8 " Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."*

## SARAKASI (SEHEMU 2)

Kurudi, wanajadiliana mbadiliko mkubwa wa maisha waliouona katika maisha ya Saulo. Wanatamani kuwa wangeona alichokiona Saulo katika kizuka ila kuona mtu akifanywa kuwa kipofu na kisha kupatiwa tena uwezo wa kuona tena ni jambo la kushangaza sana. Ajenti anatambua kuwa kama Mungu anaweza kumwokoa mtu ambaye alikuwa akijaribu na hata kuwatia gerezani Wakristo, basi Mungu anaweza kumwokoa pia. Ila kwa sababu gani? Kiongozi anajadiliana kiasi jinsi Saulo (ambaye baadaye alibadilisha jina lake na likawa Paulo) aliuzunguka ulimwengu na kuwaambia watu kuhusu Yesu na kuandika mambo mengi ambayo sasa hivi yanaitwa Agano Jipya katika Biblia! Ajenti anafurahia kuhusu mambo Mungu anaweza kuyafanya kumpitia, pia.

## HAKI

Mara nyingine, Mungu anatufanya kuzungumza na mtu kuhusu jinsi ambavyo wanamdhulumu mtu. Mambo makubwa yanaweza kufanyika tunapofuata Mwongozo wake.

## WASIFU (MWANASARAKASI)

Mtu ambaye, kwa kujitia hatari na ustadi mkubwa, anaruka, kucheza densi au kufanya mazoezi yoyote mengineyo katika kamba zilizobembea, kamba iliyokazwa n.k. kama sehemu ya maonyesho.


Majukumu: Mwanasarakasi ni msanii ambaye anaunda ratiba ambapo anaonyesha ujuzi tofauti unaohusiana na ujisawazishaji, nguvu, umakinifu na uwezo wa kuruka.

Inaweza kusemekana kuwa wanasarakasi ni mchanganyo wa sanaa na spoti. Miaka mingi kabla ya Yesu kulikuwa na watu ambao walifanya uanasarakasi, mara nyingi kwa sababu za kiibada.

Fursa: Mwanasarakasi wa Kikristo yuko na fursa ya kutenda usanii wake ili kuvutia umati mkubwa katika tukio ili kushuhudia kuhusu Mungu. Pia inawashinikiza watu walio na ujuzi huu kuwa na nidhamu na kumakinika katika kuwa na miili mizima ambako ni kuutumia wakati vinavyofaa.

Katika, uanasarakasi wa kuzoeza viungo vya mwili, ni spoti ambapo wachezaji wanashindana na kupokea matokeo tofauti. Washindani wanafaa kufanya urukaji tofauti wa uanasarakasi, ukifuatwa na mziki ambao unawaruhusu kuboresha choreografia zao. Hizi huwa zinavutia umati mkubwa na kuwezesha ushahidi mkubwa bora zaidi.

## MASWALI NA MAJIBU



1. Je, naweza kubadilika vikamilivu?

Kweli, ila iwapo tutajaribu kujibadilisha itakuwa ni misheni ambao itakuwa ni karibia isiyowezekana. Ila jambo kuu ni kuacha maisha yetu, hisia zetu na fikra zetu ndani ya Kristo Yesu. Katika njia hii tunaweza kubadilika kwa namna kamili kwa sababu nguvu yetu inamtegemea Mungu. Katika historia, tunaona kuwa Sauli alipitia mabadiliko makubwa kutoka kuwa mnyanyasaji wa kanisa hadi kuwa mtume ambaye Mungu alimtumia kwa kiasi kikubwa kushawishi ulimwengu tunaoujua na kuandika sehemu kubwa ya Agano jipya. Matendo ya Mitume yanasimulia “safari” za Paulo, Saulo akibadilika vikamilifu

2. Je, ni kwa nini kila mara huwa sielewi kitu anachoniambia Mungu?

Mungu anafanya kazi kwa namna tofauti. Ni kama vidole vya mikono yako; viko na majukumu tofauti, ila vyote vinatumika. Mara nyingine hatuelewi sababu ni kwa nini mtu anataka kufanya jambo ambalo hatuwezi

kulifanya na hatuelewi sababu ya mtazamo huu wao. Hatuwezi kujua ni nini Mungu alichomwambia huyo mtu. Kitu kama hiki kilimfanyikia Petero na Paulo. Petero hakufanikiwa sana katika kuwaambia Wayunani kuhusu wokuvu, ila Mungu alikuwa amempatia Paulo jukumu hilo.

## MAJIBU YA MAFUMBO










## MCHEZO

***kutoka upande mmoja hadi mwingine***



Mwalimu anagawanya kikundi katika safu mbili. Mwalimu anapotoa ishara, wachezaji walio katika safu ya mbele wanakimbia kuelekea upande, ili mkono wao wa kulia ukwende katika mstari wa kumalizia. Wanapofika mstari wa mwisho wanakimbia kurudi kwa upande bila kugeuka. Wanapofika kwa wengineyo katika timu, wanamgusa mchezaji anayefuata katika mstari na kusonga nyuma katika foleni. Kila mchezaji anarudia jambo hili, hadi kila mtu akimbie. Timu inayomaliza ya kwanza, itashinda.




## KAZI YA ZIADA

Liambie darasa jinsi unavyomwamini Yesu na ni nani aliyekwambia kumhusu Yesu. Iwapo ulikuwa uhubiri kuhusu Yesu, ungekuwa kasisi, mhubiri, au ungefanya shughuli nyingine.

# JE, NAWEZA KUJA PIA? 13



**Petero alihubiri wokovu: Matendo ya Mitume 2:14, 36-40**

## SARAKASI (SEHEMU YA 1)

Mchunguzi na Ajenti wanajua kamili kuwa Yesu alikufa na kufufuka na wanajua kuwa Mungu anaweza akawatumia. Ila atawatumia vipi? Kiongozi anapendekeza kuwa wanafaa kurudi katika wakati ili kuona walichofanya watume baada ya Yesu kurudi mbinguni.

## SOMO

Soma Matendo ya Mitume 2:1-14, 36-40

Petero alikuwa amekana kumjua Yesu. Sasa, alikuwa amekutana na Yesu baada ya kufufuka kwake, Yesu alikuwa amemkubali, na Petero alikuwa amejawa na roho mtakatifu wa Mungu. Hofu yake ilikuwa imebadilishwa na kuwa furaha. Uwezo huu mpya ndani ya Mungu ulimsaidia kwenda chini katika ngazi na kuzumgumza na umati. Alisema mambo magumu kwao ila aliwaeleza njia ya wokovu.

Sisi sote tumefanya mambo ambayo ni mabaya. Tumedanganyana au tumekuwa wachoyo au wabaya kwa watu wengine, mambo ambayo yanaitwa dhambi. Kwa sababu tumezaliwa katika dhambi, tunatenganishwa na Mungu, tunawekwa katika aibu na nje ya familia yake, na tunazaliwa chini ya nguvu za giza na kifo. Ila kuna habari njema! Yesu alitufia msalabani na anaishi tena! Kumwamini Yesu kuwa anavunja uwezo wa dhambi hii katika maisha yetu, kutupeleka tena hadi kwa uhusiano wa Mungu, kuondoa aibu yote na kuturudisha katika Familia yake milele na milele, na kutuweka huru kutokana na giza na kutuleta ndani ya Mwangaza wake na mamlaka yake ya upendo.

Iwapo unataka kupokea zawadi ya Mungu kupitia Yesu, hakuna maombi maalum ambayo Biblia inatwambia tunafaa kufanya, ila kitu chochote kama hichi kitafanya kazi. Yesu anakungoja kwa hamu.

*"Mungu Yesu, Nataka kukujua kwa namna binafsi. Asanti kwa kunifia katika msalaba kwa dhambi zangu. Nafungua mlango wa maisha yetu na kukupokea kama Mwokozi wangu na Mungu. Asanti kwa msamaha wako wa dhambi zangu na kunipa maisha ya milele na milele. Kuwa mdhibiti wa maisha yangu. Nifanye kuwa mtu ambaye ungependa niwe."*

Iwapo umeomba maombi haya, kuna sherehe kubwa mbinguni!

## AYA YA KUMBUKUMBU

*Yohana 3:16 " Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."*

## SARAKASI (SEHEMU YA 2)

Timu inaporudi, inahisi furaha tele. Wamemwona Petero, mvuvi ambaye hajasoma ambaye alimkataa Yesu, simama na kuzungumza mbele ya umati mkubwa. Kiongozi anawatia moyo Ajenti na Mchunguzi, kwa kuwaambia kuwa mtu yeyote anayemwamini Yesu anapata Roho mtakatifu pia, kama walivyokuwa watume, na atawawezesha kuzungumza kwa namna ya ujasiri au kuitumikia kanisa na watu wa Mungu kwa namna zozote ambazo tuko bora katika. Mkaguzi tayari yuko bora katika kuwasaidia watoto wachanga na kupata marafiki wapya kutoka mataifa mageni.
Ajenti anaijenga biashara yake ndogo kwa mapambo ya kuning'inizwa ukutani na kila mara huwa anataka kujijuza na kujaribu kujua jinsi mambo yalivyo. Wote wawili wameona vitu vizuri kutoka kwa maisha ya Yesu. Kwa usaidizi wa Roho mtakatifu wanaweza kutumia mambo haya yote kuwaambia watu kuhusu Yesu na kuwaalika watu kumkubali Yesu katika maisha yao, pia!

## HAKI


Mungu anakupenda sana hata ALIKUPA mwana wake wa pekee ili uwe na maisha ya milele na milele! Wacha tuwaonyeshe wengine upendo huu kwa kujitolea kwao.

## WASIFU (MVUVI)

Mvuvi ni mtu ambaye anapata mapato yake kwa kuwashika samaki na wanyama wengine wa majini. Wanajaribu kuvua wa kutosha ili kujilisha na kuuza. Ni ajira ambayo imekuwepo tangu kuanza kwa maisha ya mwanadamu.

Majukumu: Wavuvi wanakwenda katika ziwa kuvua samaki na kurudi na samaki na samakigambi. Vikundi vya kufanya uvuvi vimeundwa na watu walio na kazi na majukumu tofauti. Kazi ni kushughulikia vifaa, kuongoza boti baharini, kupanga samaki waliovuliwa, kuwaweka katika mikebe iliyo na barafu, mara nyingine kuwachinja samaki (huwezi kumchinja pweza vizuri sana), na kuwapeleka katika soko.

Fursa: Mvuvi wa Kikristo ako na fursa ya kushirikiana vizuri na kikosi chake, kuwa mwaminifu kuhusu maeneo ya kufanya uvuvi na samaki waliowavua, na kufanya haki kuhusu bei wanaowatoza wananuzi. Wanaifanyia jamii huduma nzuri kwa sababu samaki ni mlo mkuu kwa watu wengi na huwa ni za bei nafuu na lishe bora lenye afya.



## MASWALI NA MAJIBU

1. Je, ni vigumu sana kuhubiri katika umma?


Hili ni kulingana na tabia ya kila mtu. Ili kuhibiri katika umma, tunafaa kujitayarisha kwa kusoma Biblia na kutayarisha mada ambazo zinawafunza watu. Kuna watu ambao wanapata ugumu wa kuzungumza na mtu mmoja kibinafsi badala ya kuzungumza na umati na kusambaza neno la Mungu. Baada ya muda, tunajifunza jinsi tunatenda vinavyofaa katika uhubiri.


2. Je, ni kwa nini hata nikijuta jambo huwa nalirudia?

Sisi ni wanadamu na hatuna nguvu ya kuondoa mambo ambayo yalituumiza au kumkasirisha Mungu. Hata hivyo, Mungu anaweza kutupa nguvu katika maeneo ambapo tuko dhaifu. Tunaweza kufanya mambo kwa majuto, ila pole kwa pole, Mungu anaweza akatufanya kuwa wenye nguvu.

## MAJIBU YA MAFUMBO











## MCHEZO

***Asiachilie vifundo vya miguu yako***

Mwalimu anawagawanya wanafunzi katika mistari mitatu au minne. Ishara itakapotolewa, kila wachezaji wanaoongoza watagusa kila kifundo cha miguu yao kwa kila mkono na kuendelea kushikilia vifundo huku wakitembea haraka wawezavyo hadi wafikie lengo na kumrudia mchezaji mwingine. Iwapo mchezaji ataachilia kifundo chake au kuanguka, wanafaa kurudi katika eneo walikoanzia. Timu inayomaliza kwanza inashinda.






## KAZI YA ZAIDA

Iwapo utakumbuka ukimdanganya mtu hivi majuzi, jaribu kuzungumza na huyu mtu na kumwomba msamaha.